

TOLEO MAALUM

UQAB
Jarida la

Toleo 22 - Safar 1440 H / Novemba 2018 Miladi

Kampeni ya Kimataifa:
“Familia: Changamoto Na Suluhisho La Kiislamu”
iliyo Zinduliwa na Kitengo cha Wanawake Katika
Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir



Familia
CHANGAMOTO NA
SULUHISHO LA KIISLAMU

Kampeni ya Kimataifa: “Familia: Changamoto na Suluhisho la Kiislamu” iliyo Zinduliwa na Kitengo cha Wanawake Katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir



Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Mnamo 3 Oktoba, Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir kilizindua kampeni muhimu ya kiulimwengu kwa anwani, “Familia: Changamoto na Suluhisho la Kiislamu” ambayo itamalizikia katika kongamano la kimataifa la wanawake mwishoni mwa Oktoba litakalo hudhuriwa na wazungumzaji kutoka pembe zote za dunia.

Miundo imara, yenye umoja wa familia ndio kitovu cha mujtamaa imara, zisotingishika, na zenye mafanikio. Ni muhimu mno katika utoaji usaidizi wa kimwili, kihisia, na kimada na kuwepo kwa hali nzuri ya wanachama wake wote na kuhakikisha uchungaji thabiti na ulezi mwema wa watoto. Lakini, leo kuna mgogoro unaoathiri utulivu na umoja wa maisha ya ndoa na familia katika jamii kote duniani, ikiwemo ndani ya biladi za Kiislamu. Kuingizwa kwa thaqafa ya kimagharibi katika ulimwengu wa Kiislamu, pamoja na uharibifu wa uhuru zake za kijinsia zisizo na mipaka, muozo wa nyendo za ubinafsi za kimaisha, maadili ya kimada ya kirasilimali na mtafaruku wa fahamu za utetezi wa kijinsia kama vile usawa wa kijinsia, kupitia majukwaa kama vile sekta ya burudani, nidhamu za elimu, mitandao ya kijamii, na mashirika ya utetezi wa kijinsia yameharibu na kumomonyoa taasisi ya ndoa na kusababisha janga la kuvunjika kwa familia. Hii imechochewa na kupitia kuwepo kwa mila za Kiarabu, Kihindi, au Kiafrika zisizokuwa za Kiislamu ndani ya jamii zetu za Kiislamu zinazobeba mitazamo na vitendo vyenye madhara ambavyo vimesababisha mizozo katika maisha ya ndoa na familia. Yote haya, pamoja na ukosefu wa ufahamu safi wa sheria za kijamii za Kiislamu, yamepelekea matarajio maovu katika ndoa, kusababisha kuchanganyikiwa kuhusiana na dori na haki za waume na wake katika maisha ya ndoa na familia, na kupelekea ongezeko kubwa la mahusiano nje ya ndoa, ghasia za kinyumbani na talaka katika jamii za Kiislamu kote duniani. Hii ni pamoja na kusababisha kurefuka kwa umri wa kuoa, kudunishwa kwa cheo cha mama na mgogoro wa uwezo wa kuzaa kutokana na wanandoa kuchagua kuwa na watoto wachache. Kuvunjika huku kwa maisha ya familia katika biladi za Kiislamu kumechangiwa na utawala fisidifu wa serikali za kisekula zisokuwa za Kiislamu katika eneo hilo kupitia upigaji debe na utekelezaji wa maadili huru, ya kisekula ya kirasilimali, sera, sheria na nidhamu zinazoeneza fikra na miondoko michafu ya kimaisha ndani ya mujtamaa zao. Fauka ya hao, serikali hizi, pamoja na serikali za Kimagharibi, mashirika ya kimataifa kama UN na harakati za utetezi wa kijinsia zimejiingiza katika mvutano mkubwa ili kubadilisha zaidi familia ya Kiislamu na sheria za kijamii kwa misingi ya uhuru ya kisekula pamoja na kuimarisha maadili huru ya kijinsia na usawa ndani ya jamii za Kiislamu mbazo tayari zishapanda mfadhaiko wa kijamii ndani ya madola. Hali ya kiungo cha familia ndani ya Ummah wa Kiislamu hivyo basi inafuata njia hiyo hiyo ya kimakosa kuelekea katika maangamivu yanayoonekana Magharibi ambako muundo wa familia unayeyuka. Hii ni licha ya kuwa nguvu, umoja na utulivu wa maisha ya familia mwanzoni ilikuwa ni sifa kuu ya Ummah wa Kiislamu.

Ukosefu wa furaha, kuvunjika na kutofanya kazi kwa maisha ya ndoa na familia imesababisha machafuko makubwa ya kihisia kwa wote waliomo na huenda ikawa na athari mbaya zaidi juu ya watoto, watu binafsi na mujtamaa. Hivyo basi ni muhimu sana kutiliwa maanani na kuwa makini katika kuzungumziwa mgogoro huu katika kiungo cha familia na kuiokoa kutokana na maangamivu. Katika kampeni na kongamano hili muhimu, tutaangazia hatari za mabadiliko ya sura ya muundo wa familia katika ulimwengu wa leo. Tutatambulisha mambo makuu yanayodhuru taasisi ya ndoa na utulivu wa maisha ya ndoa, ikiwemo dori ya vyombo vya habari na serikali katika kukoleza mgogoro huu. Tutafichua ajenda za kitaifa na kimataifa za kutia usekula katika familia za Kiislamu na sheria za kijamii ili kuwaeka mbali zaidi Waislamu kutokana na Dini yao. Na muhimu vile vile, tutaangazia nidhamu ya kijamii ya Kiislamu na kuonyesha jinsi mtazamo wake wa kipekee katika kupangilia mahusiano ya kijinsia, kwa misingi yake sahihi, maadili na sheria, ukiwemo ufafanuzi wake wazi wa majukumu ya wanaume na wanawake ndani ya maisha ya familia, unavyo weza kulinda ndoa, kukuza utulivu na maelewano ndani ya maisha ya ndoa, kunyanyua cheo cha mama katika hadhi kuu inachostahiki na kuasisi na kuhifadhi viungo vya familia imara zilizo na umoja. Kampeni na kongamano hili pia litafanua dori muhimu mno ya usimamizi wa Kiislamu chini ya dola ya Khilafah iliyojengwa juu ya Utume katika kukuza, kupigia debe na kulinda viungo imara vya ndoa na familia ili kuonyesha namna gani Uislamu kihakika ndio ngome ya familia!

Kampeni hii yaweza kufuatiliwa katika: <http://www.hizb-ut-tahrir.info/en/index.php/dawah/cmo/16024.html>

Ukurasa wa Facebook: www.facebook.com/WomenandShariah

Dkt. Nazreen Nawaz
Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake
Katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

“Enyi Mabarobaro! Yeyote Mwenye Uwezo Miongoni Mweni Basi na Aoe”



Allah (swt) aliwaumba wanadamu na kuifanya ndoa kuwa njia ya kuongeza kizazi; Allah (swt) aliita ndoa katika Quran “ahadi madhubuti” ili kuashiria umuhimu wake. «وَأَخَذْنَا مِنْكُمْ مِيثَاقًا غَلِيظًا...» na wao wanawake wamechukua kwenu ahadi iliyo madhubuti?” [An-Nisa’: 21]

Mtume (saw) alimkemea kila yule anayekataa kuoa kwa sababu yoyote ile, hata kama sababu hii ni Qiyam ul-Layl (kusimama usiku kwa ajili ya ibada) au kufunga. Mtume (saw) amesema: «وَأَتْرُوجُ النِّسَاءَ، فَمَنْ رَغِبَ عَن سُنَّتِي فَلَيْسَ...» “...na mimi naoa wanawake, basi yeyote anaye kwenda kinyume na Sunnah yangu si katika mimi.”

Imam Ahmad (Rahimahullah) amesema: “Kukataa kuoa si katika Uislamu, yeyote anaye kushauri usioe; amekulingania kwa chengine kisichokuwa Uislamu”.

Kuzembea katika kuoa ni kinyume na Sunnah, na kinyume na umbile asili; na mlango wa kueneza ufasidi na uchafu, na maovu, Allah utuepushe. Kujiweka mbali na ndoa pasi na sababu halali hupunguza wasiwasi na kutoridhika, kwa sababu ndoa huleta utulivu, amani, kujali na mapenzi.

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

“Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mupate utulivu kwao. Na amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa wanao fikiri.” [Ar-Rum: 21]

Ndoa hukubaliana na umbile la mwanadamu na huhakikisha kuendelea kubakia kwa wanadamu, urithi duniani, kuongezeka kwa vizazi, na ufanisi katika ardhi; hutimiza ahadi ya Mtume (saw) ya kuongezeka kwa idadi ya uzaanaji (wa Umma huu) mbele ya mataifa mengine siku ya Qiyama.

Lakini tunapouangalia Ulimwengu wa Kiislamu, tunaona idadi kubwa ya wanawake na wanaume wadogo ambao hawako ndoani, na utafiti wa hivi majuzi waonyesha kuwa thuluthi moja ya idadi ya wanawake wadogo ambao hawajaolewa katika biladi za Kiarabu wamefikia umri wa miaka 30. Kwa mfano, asilimia ya wanaume ambao hawajaoa nchini Misri wa kati ya umri wa miaka 18 na 29 ilikuwa takriban asilimia 37.4 ya idadi jumla ya watu, ikilinganishwa na asilimia 16.4 ya wanawake katika sensa ya 2017, kwa mujibu wa takwimu ya sensa ya Misri. Kwa mujibu wa baadhi ya takwimu, Palestina ilipata asilimia ya chini kabisa ya asilimia 7, Bahrain asilimia 25, Yemen asilimia 30, Kuwait, Qatar na Libya asilimia 35, Misri na Morocco asilimia 40, Saudi Arabia na Jordan asilimia 45, Algeria asilimia 51, Tunisia asilimia 65, Iraq na Syria asilimia 70, Imarati asilimia 75, huku Lebanon ikirekodi asilimia kubwa zaidi ikifika asilimia 85. (Albawaba)

Asilimia hizi kubwa si za kuridhisha, zinazopelekea maovu, fitna na kupotoka, yanayoathiri familia na mujtamaa. Na hawa vijana wadogo hudhani kuwa wanaishi maisha ya utulivu kando na matatizo ya kifamilia na kwamba maisha yao yako huru na hofu na matatizo ya kifamilia, lakini wamekosea kwa sababu ikiwa watajizua nafsiya zao, wataishi kwa fadhaido,

Endelea Uk..4

JARIDA LA
UQAB

wasiwasi na kuteseka kwa maisha ya uchungu na watanyimwa starehe ya ndoa na neema ya watoto ambayo ni neema kubwa zaidi ambayo Allah amewapa wanadamu. Ikiwa hawatajuziwa nafsiya zao, watageukia haramu na madhambi, kuachana na Dini, maadili mema, na usafi wa tabia.

Kwa sababu hii, sababu za kucheleweshwa kwa ndoa au kujiepusha nayo zinapaswa kuangaliwa kwa makini ili kuondoa vikwazo hivyo na kuwasahilishia hili vijana wa kiume na wa kike. Vyenginevyo, Haram itabadilishwa kuwa Halal, na ufisadi, zinaa na madhambi yataenea katika familia na mujtamaa, na Umma utawekwa mbali na mwamko na kurudi tena kwa Uislamu; katiba, njia na dola yake.

Ikiwa tutaangalia sababu za kucheleweshwa kwa ndoa, tutaona kuwa wakati mwingine zinatofautiana kutoka nchi moja hadi nyengine, lakini asili yake ni moja nayo ni kutotekelezwa kwa hukmu za kisheria, miongoni mwa sababu hizi kubwa ni:

Gharama kubwa ya mahari na gharama kubwa ya ndoa katika mambo yasiyo na umuhimu, yanaifanya ndoa kuwa ngumu au kukaribia kutowezekana kwa vijana wengi nayo hupelekea kuicheleweshwa, au hugeuka kuwaoa wanawake wa kigeni ambao haiwagharimu wao chochote, ambapo huongeza idadi ya wanawake ambao hawajaolewa. Hili ni kinyume na lile ambalo Allah amelipanga ili kurahisisha gharama za ndoa. Mtume (saw) amesema, «أَعْظَمُ النِّسَاءِ بَرَكَةً أَيْسَرُهُنَّ مَنُونَةٌ» “Wanawake wenye Baraka nyingi zaidi ni wale walio na mahari ya chini kabisa.”

Hii ni bila ya kutaja masharti mengi na matakwa ya kimada ya vijana wa kike na familia zao, na kutilia maanani upande wa kimada katika uchaguzi wa mume na kutotilia maanani sifa nyenginezo muhimu kama Dini, tabia na uwezo. Ash-Shari’ alisisitiza kuangalia sifa mbili kuu katika mume. Mtume (saw) amesema: «إِذَا آتَاكُمْ مِنْ تَرْسُونَ دِينَهُ وَخُلُقَهُ فَرُوجُهُ إِلَّا تَفْعَلُوا تَكُنْ فِتْنَةً فِي الْأَرْضِ» “Atakapo wajilieni yule ambaye mumeridhia Dini na akhlaqi yake basi muozeni! Ikiwa hamutafanya hivyo kutakuweko na fitna katika ardhi na ufisadi mkubwa” [Tirmidhi]

Hapana shaka kuwa Allah amedhamini kuwasaidia waja wake waumini ili waowane, Mtume (saw) amesema: «ثَلَاثَةٌ حَقٌّ عَلَى اللَّهِ عَوْنُهُمْ: الْمَجَاهِدُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمُكَاتِبُ الَّذِي يُرِيدُ الْأَدَاءَ» «وَالنَّاسِحُ الَّذِي يُرِيدُ الْعُقَافَ» “Watu watatu Allah ni haki awasaidie: anayepigana Jihad katika njia ya Allah, na mtumwa ambaye anataka kujikomboa, na yeyote anayetaka kuhifadhi nafsiya yake kwa ndoa.” [Tirmidhi]

Inashangaza sana kumpata mtu amemuozesha binti yake kwa mtu asiye swali na asiye muogopa Mola wake, kwa ajili ya mali yake na wingi wa pesa zake na kumkataa mtu mwema kwa ajili ya umasikini wake!! Tatizo hili linachochea zaidi na kukosekana dola ya

Kiislamu ambayo ingechunga mambo ya watu, na kwa mfumo wa kirasilimali ambao tunaishi ndani yake, kama vile kuenea kwa ukosefu wa ajira, mapato ya chini, kuenea pakubwa kwa ufisadi na ubaguzi wa kikabila, ambayo huwafanya wale wanaotaka kuoza kushindwa kuanzisha maisha ya familia.

Miongoni mwa vigezo muhimu vinavyozuia ndoa na kuicheleweshwa kwa vijana wengi wa kiume na wa kike ni athari ya vyombo fisidifu vya habari vinavyo ongozwa na kushawishiwa na fahamu za Kimagharibi, fikra zake msingi, miondoko ya kijamii, fikra na mitazamo iliyo mbali na sheria za Uislamu; ambayo husambazwa kwa watoto wa Kiislamu kupitia katika musalsala tofauti tofauti, filamu na vipindi. Hii ni ikiongezewa na udhaifu wao katika kushikamana na dini na kukosekana kwa sheria na mipaka katika nidhamu hii inayopelekea kuporomoka kwa maadili na akhlaqi, na uwazi usio na mipaka. Hivyo basi, baadhi wameanzisha mahusiano haramu na kutafuta matakwa yaliyo haramishwa na ndoto hadaifu na mangati ya mapenzi feki na haja ya wapenzi kuwa na uhusiano kabla ya ndoa ili wajuane!! Hii ni mojawapo ya fitna kubwa, Allah atuhifadhi, au hamu yao ya uhuru na wala sio kutenda kwa uwajibikaji au kukinai kwengine kiakili kusiko kuwa na dalili katika sheria na kusikopaswa kutegemewa.

Kutokana na kanuni zilizotungwa na kibinadamu za kirasilimali katika biladi za Kiislamu, ambazo zinatawaliwa kwa manufaa na maslahi, na ambapo mahusiano ya kifamilia na ulezi sahihi na mafungamano ya kifamilia yameyeyuka, idadi ya wanawake wadogo huhisi kutishika na hofu ya mustakbali. Hivyo basi, kwa mujibu wao watatafuta silaha ya kulinda mustakbali wao; nayo ni elimu na kazi, hata kama itagongana na ndoa yao na cheo chao cha mama. Lau hukmu za Kiislamu zingetekelezwa, hawange hisi hivi kwa sababu Uislamu unadhamini ulinzi, uangalizi na usalama wao katika dori zao zote maishani. Pia ni lazima tuisahau hadaa ya usawa na uwezo wa kiuchumi, inayo wafanya wanawake kufikiria uhuru na kutafuta mafanikio na shakhsiya yao ya kibinafsi kupitia kutafuta umaarufu katika mujtamaa, na hivyo basi fikra ya tabaka na usawa wa kitamaduni kuibuka kati ya wanandoa na kuwa kipimo cha wanawake kukitumia kuchagua mtu wa kuolewa naye, huenda kisipatikane, na kupelekea kucheleweshwa kwa ndoa au kutoa kabisa. Wakati mwingine familia ndio sababu ya kuchelewa kwa ndoa ya binti yao au kutekeleza “Al Adhl” (kuzuia mabinti kuolewa) ili kufikia matakwa yao na kunufaika kimada.

Ili kutatua tatizo au kupunguza athari yake ni lazima tuondoe sababu zake, ni lazima tuanze kusisitiza umuhimu wa ndoa na udharura wake kwa vijana wa kiume na wa kike, na ni lazima tuonyeshe hatari za kuepukana na ndoa au kuifanya kuwa ngumu. Na kisha ni lazima tufanye kazi ili kusahilisha ndoa kupitia yafuatayo:

Kupunguza gharama za ndoa, kupunguza mahari, kupunguza matakwa ya ndoa, na kuwakubali wale tuliowakinai Dini na akhlaqi zao, hata kama wanapesa kidogo, na kwa kuzingatia maneno ya Allah (swt):

وَأَنْكَحُوا الْأَيَامَىٰ مِنْكُمْ وَالصَّالِحِينَ مِنْ عِبَادِكُمْ وَإِمَانِكُمْ إِنْ يَكُونُوا فُقَرَاءَ يُعْطِهِمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ

“Na waozeni wajane miongoni mwenu na wema miongoni mwa watumwa wenu na wajakazi wenu. Wakiwa mafukara Allah atawatajirisha kwa fadhila zake. Na Allah ni Mwenye wasaa na Mjuzi.” [An-Nur: 32]. Na Hadith ya Mtume (saw):

«إِنَّ مِنْ يُمْنِ الْمَرْأَةِ تَيْسِيرَ خَطْبَتِهَا، وَتَيْسِيرَ صَدَاقِهَا، وَتَيْسِيرَ رَجْمَتِهَا»

“Hakika katika Baraka ya mwanamke: ni wepesi wa posa yake, na wepesi wa mahari yake, na wepesi wa kizazi chake (kushika mimba na kuzaa kwake).”

Na katika maneno ya Umar (ra) amesema: “Musiongeze mahari ya wanawake, lau kama ingekuwa ndio utukufu wa Dunia na Akhera au ingekuwa ni uchaMungu wa Akhera basi Mtume wa Allah angestahiki zaidi hilo kuliko nyinyi (lakini Yeye (saw) hakuongeza mahari).” [Imesimuliwa na wapokezi watano na kuthibitishwa na Tirmidhi]

Na sisi twamwambia yule anayemzuia binti yake au dadake kuolewa, kutokana na tamaa ya pesa au kazi yake, licha ya kupata posa kutoka kwa mwanamume mwema na kukubali kwao posa hiyo: kwamba hili limeharamishwa na sheria. Allah (swt) asema:

فَلَا تَعْضُلُوهُنَّ أَنْ يَنْكِحْنَ أَزْوَاجَهُنَّ إِذَا تَرَاضَوْا بَيْنَهُمْ بِالْمَعْرُوفِ

“...basi musiwazuie kuolewa na waume zao (watalaka wao) endapo baina yao wamekubaliana kwa wema” [Al-Baqara: 232].

Ama kuhusu vijana waliozembea katika ndoa kwa sababu ya fikra na fahamu potofu ambazo ziko mbali na Uislamu, tunawaambia: Muogopeni Allah na mujue kuwa wakati unapita na matamano yanamalizika na kujilaumu na huzuni pekee ndio zitasalia, na utulivu na amani zitakuja pekee kupitia kuoa mwanamke mwema au mume mwema.

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

“Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mupate utulivu kwao. Na amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa wanao fikiri.” [Ar-Rum: 21]

Na wala musiiige kile mukionacho katika musalsala na vipindi haribifu vilivyojaa fahamu na suluki fisidifu zilizo mbali na Dini, akhlaqi na maadili yenu, ambavyo vimeletwa kwetu ili kutufisidi, kwa sababu wanaogopa kurudi tena kukubwa kwa Uislamu kama ulivyokuwa wakati wa zama za kuwepo dola yake imara.

Ama kwa wewe, binti yangu na dadangu, unapaswa kumkubali mume anayemridhisha Allah na Mtume wake, na wala usifadhilishe asiyekuwa na uwezo kwa mwenye uwezo kwa ajili ya pesa au jina au cheo unachokitaka, au kwa fadhila unazozitaka, au kwa matarajio ya kidunia, ili upate Baraka za Allah. Vilevile, masomo au kazi yako si muhimu kuliko ndoa yako na cheo chako cha mama, na hakuna mgongano baina ya hayo, ikiwa utaweza kuweka mizani kati ya hayo. Dori yako ya kwanza katika maisha haya ni kuwa mama na mke nyumbani, na kutafuta pato ni jukumu la mwanamume (mume). Ni lazima atimize mahitaji yako yote. Hili halipunguzi cheo na hadhi yako, bali kinyume chake, hii ni dori yako na Wallahi ni dori muhimu sana, na miongoni mwa majukumu magumu ambayo wanaume hawawezi kuyafanya, ni kumjenga mwanadamu, nyumba yako na familia yako haviwezi kufidiwa na cheti au kazi au chochote.

Hapa tungependa pia kuzindua kuhusu hukmu ya kisheria kuwa kukosekana kwake kumepelekea ongezeko la idadi ya wanawake ambao hawajaolewa. Hukmu hii iliharibiwa kwa musalsala, filamu uandishi duni wa waandishi duni wa kiume na wa kike; hii ni familia ya wake wengi, ambayo ni hukmu ya sheria kutokana na hukmu za Allah na kutokana na Sunnah ya Mtume (saw), ambayo ni suluhisho zuri la ongezeko la idadi ya wanawake ambao hawajaolewa, twahitaji kufafanua sheria hii. Vilevile mwenye wake wengi ni lazima amche Allah na kuhakikisha uadilifu, kilicho haribu sheria ya wake wengi ni kukosa uadilifu kwa wenye wake wengi. Wengi wao huegemea kwa baadhi ya wanawake (wake) na watoto wao kwa gharama ya wanawake (wake) wengine na watoto wao, hili liliwafanya wanawake kuchukua uke wenza na wengine wengi wanaogopa hili kwa nafsi zao na binti zao. Baadhi yao wafadhilisha kubaki bila ya kuolewa kuliko kuolewa na mtu mwenye wake ambaye huenda akakosa uadilifu kwake au kwa mke mwengine kwa sababu yake kwa kuhisi kuwa dhambi.

Na tunatamatisa kwa maneno ya Mtume (saw):

يَا مَعْشَرَ الشَّبَابِ، مَنْ اسْتَطَاعَ مِنْكُمُ الْبَاءَةَ فَلْيَتَزَوَّجْ، فَإِنَّهُ أَعْصَمٌ لِلْبَصْرِ وَأَحْصَنُ لِقَرْجٍ، وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَعَلَيْهِ بِالصَّوْمِ، فَإِنَّهُ لَهُ وَجَاءٌ

“Enyi Mabarobaro! Yeyote Mwenye Uwezo Miongoni Mwenu Basi na Aoe, kwani hakika yake ni huziba macho na kuhifadhi tupu (kutokana na zinaa), na ambaye hana uwezo basi ni juu yake kufunga, kwani hakika saumu ni kinga kwake.”

Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

Muslimah Ash-Shami (Umm Suhaib)

“Kuyeyuka kwa Familia” za Mujtamaa wa Kisekula wa Kimagharibi

SEHEMU 1: Uhakika wa Kuyeyuka kwa Familia katika Dola za Kisekula za Kimagharibi

Mnamo Aprili 2008, Hakimu Paul Coleridge, jaji anaye husika na mahakama za kifamilia kote Kusini Magharibi mwa Uingereza, alitoa hotuba kwa mawakili wa familia kutoka katika shirika la “Resolution”, ambapo aliyasifu maisha ya familia nchini Uingereza kuwa ni “yenye kuyeyuka” yakidhihirisha janga la kuvunjika kwa familia. Alisema: “Idadi kubwa ya familia sasa zina watoto wanaolelewa na kina mama ambao wana watoto kutoka kwa mababa tofauti tofauti, hakuna yeyote kati yao anayechukua nafasi katika maisha yao au kuwasaidia au kuwalea... Hizi sio kesi kando, za kipekee. Ni sehemu ya shehena za kesi katika mahakama za kifamilia.” Aliendelea, “Takriban maovu yote ya kijamii yanaweza kunasibishwa moja kwa moja na mporomoko wa maisha ya familia. Sote twajua hili. Tathmini asili ya kila mtoto katika nidhamu ya uangalizi au nidhamu ya uadilifu wa vijana na utagundua familia iliyo vunjika. Ditto mraibu wa mihadarati. Ditto mlevi. Ditto wale watoto watoro au watundu shuleni. Chimba kesi hizi na utapata familia iliyo na matatizo, yaliyotokana na uhusiano wa wazazi ulio haribika na kuvunjika – au usio kuwako kamwe.”

Wasifu huu mbaya wa maisha ya familia nchini Uingereza umejiri baada ya kutokea habari nyenginezo, ikiwemo kuanguka kwa viwango vya ndoa nchini Uingereza na Wales na kufikia kiwango cha chini kabisa tangu rekodi zianze kuwekwa mnamo 1862 (Afisi ya Takwimu za Kitaifa (ONS)) na ongezeko la viwango vya juu zaidi vya talaka tangu mnamo 1996. Maoni haya kuhusiana na kuyeyuka kwa muundo wa familia nchini Uingereza pia yalakaririwa na wengi wa wanasiasa, wasomi na walimu nchini humo. Robert Wheelan kutoka katika taasisi ya wachambuzi wakuu ya CIVITAS (Taasisi ya Utafiti wa Mujtamaa wa Kijamii), ambayo aghalabu huishauri serikali ya Uingereza juu ya maswala ya kijamii, ilieleza kuwa kuvunjika kwa familia ni tatizo kubwa mno kwa dola kusaidia kutatua. Alisema, “Dola huenda ingeweza kumwaga pesa na kuwapa watoto usaidizi kama ingekuwa kiwango cha familia zilizo vunjika ni kidogo, lakini haiwezi kulimudu tatizo lenye uzani mkubwa kiasi hiki.” Karen Woodall kutoka katika kituo cha familia zilizo tengana alitoa maoni, “Kutengana kwa familia hakika ndio ukweli wa maisha nchini Uingereza na katika mujtamaa zote. Ikiwa utaongezea mababu na nyanya wa watoto ambao wazazi wao wametengana na wa wazazi walio katika mahusiano na wazazi wengine waliotengana, ni wazi kuwa talaka na kutengana ndio kadhia inayo athiri nusu ya idadi hii.” Na walimu katika kongamano la 2008 la kila mwaka la Shirikisho la Walimu na Wahadhiri lilieleza kuwa “duara la sumu” la kuvunjika

kwa familia ndilo linalo athiri uwezo wa watoto kusoma, afya yao ya akili na hali zao jumla.

Kwa zaidi ya muongo mmoja uliopita, mizani ya kuyeyuka kwa kiungo cha familia nchini Uingereza imeongezeka zaidi. Ukweli ni kuwa, kimekuwa katika mporomoko pasi kizuizi. Christian Guy, Mkurugenzi wa Kituo cha Haki cha Kijamii (CSJ), mchambuzi mkuu wa Kiingereza mwenye ushawishi anaye shauri juu ya maswala ya kijamii nchini Uingereza, alionya katika ripoti iliyo chapishwa mnamo 2013, kwa anwani, “Familia zilizo vunjika: Ni Kwa Nini Ustawi ni Muhimu”, kuhusu “‘tsunami’ ya kuvunjika kwa familia inayo ishambulia nchi hii”. Alitaja kuwa mwanadamu, jamii na gharama za kifedha ‘zina athari’ kwa watoto na vile vile watu wazima licha ya kukabiliwa na ‘dharura’ hii ya kitaifa, majibu kutoka kwa wanasiasa wa upande wa kushoto na kulia yamekuwa finyo.

Tsunami hii ya kuvunjika kwa familia inamulika dola zote katika ulimwengu wa magharibi. Nchini Uingereza, kiwango cha talaka kinasimama katika asilimia 42 (ONS). Mnamo 2012 kulikuwako na talaka 13 kila saa moja nchini Uingereza na Wales. Nchini Amerika asilimia 53 ya ndoa humalizikia kwa talaka, nchini Sweden ni asilimia 64, na nchini Belgium ni cha kushtua macho cha asilimia 70 (tarakimu kutoka Business Insider). Kwa mujibu wa shirika la Eurostat, kati ya 1965 hadi 2013 kiwango jumla cha talaka kiliongezeka katika nchi 28 za Umoja wa Ulaya (EU).

Ongezeko hili kubwa la talaka limefuatiwa na ongezeko kubwa la familia zenye mzazi mmoja – familia ambazo mtoto anaishi na mamake au babake pekee. Nchini Uingereza, kati ya 1996 na 2012 idadi ya familia zenye mzazi mmoja ziliongezeka kwa asilimia 25 hadi kufikia milioni 2 na sasa inawakilisha robo ya ‘familia’ zote zenye watoto wanaozitegemea (ONS). Ukweli ni, kwa mujibu wa tarakimu za serikali, takribani nusu ya watoto wote wenye umri wa miaka 15 nchini humo hawaishi na wazazi wao wote wawili wa kuwazaa. Katika jamii masikini zaidi, hii inaongezeka hadi 2/3 ya matineja hao. Idadi kubwa zaidi (asilimia 92) ya familia zenye mzazi mmoja zilizo na watoto wenye kuzitegemea zinaongozwa na kina mama; wengi waking’ang’ana kuwalea watoto wao peke yao, huku pia wakiwa watafutaji riziki peke yao wa familia zao. Kila mwaka kuna ongezeko la watu 20,000, wengi wao wakiwa wanawake, wanajiunga na wale wanaolea watoto peke yao. Natija yake ni idadi kubwa ya watoto nchini Uingereza, 1 kati ya 3, anakuwa

Endelea Uk..7

pasi na baba nyumbani, huku ikikadiriwa kuwa milioni 1 hadi 2 yao wananyimwa mawasiliano ya maana na baba zao (ONS), na wengine wao wakiwa hawana mawasiliano kabisa. Tarakimu rasmi za usajili wa uzazi za 2015 zinaonyesha kuwa zaidi ya nusu ya kina mama wenye watoto matineja hawaishi na baba au jina la baba halikusajiliwa. Taasisi ya Mababa yaeleza kuwa kufikia wakati wanafika umri wa miaka 16, 1 kati ya 6 ya watoto wote nchini Uingereza huwa hajawahi kumuona baba yake kamwe. Davidi Cameron, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza, alisema katika hotuba yake katika Kongamano la Chama cha Conservative kuwa, “Leo, tineja anayeketia mitihani ya GCSE kuna uwezekano zaidi wa kumiliki simu ya smartphone kuliko kuwa na baba anayeishi nao.”

Hadithi hii ndiyo iliyoko katika dola nyenginezo za kisekula za Kimagharibi. Kwa mujibu wa zoezi la Usajili watu la Amerika ya 2010, 1 kati ya watoto 3 nchini Amerika (milioni 15) wanaishi pasi na baba na takriban milioni 5 wanaishi pasi na mama. Na katika baadhi ya sehemu za mijini, ni 1 kati ya watoto 10 pekee ambaye baba yuko.

Sambamba na janga hili la kuvunjika kwa familia ndani ya mujtamaa za Kimagharibi, kumekuweko na kushuka kwa viwango vya hali ya juu vya ndoa ndani ya nchi hizi kwa zaidi ya miongo michache iliyopita. Kwa mujibu wa Eurostat, kati ya 1965 na 2013, kiwango jumla cha ndoa katika nchi 28 za EU kimeporomoka kwa karibu asilimia 50 kwa tathmini ya juu juu. Nchini Uingereza, kwa zaidi ya miaka 40 iliyopita, kiwango cha idadi ya watu wazima ambao wamo ndani ya ndoa kimepungua kutoka asilimia 70 ya idadi ya watu hadi zaidi ya nusu (CSJ). Mwaka 2013 ulinakili kiwango cha chini zaidi cha ndoa. Kwa mujibu wa ONS, ni nusu ya matineja leo pekee nchini humo ambao wataoa. Katika nyingi ya nchi za Nordic kama vile Iceland, Denmark, na Norway, ni asilimia 30 pekee ya wanawake wameolewa, huku kiwango hicho kikishuka kuwa kichache zaidi ya asilimia 20 kwa wale wanawake walio na umri kati ya 25 na 29. (worldatlas.com)

Kinyume na kushuka huku kwa viwango vya ndoa, watu kuishi pamoja nje ya mafungamano ya ndoa ndani ya dola za Kimagharibi imeongezeka pakubwa mno huku ikitambuliwa ndani ya mujtamaa huru kama ‘muundo wa familia’ unaokubalika, na kuwa sambamba kimaadili mithili ya taasisi ya ndoa. Kwa hivyo, nchini Uingereza, huku wachache zaidi ya 1 kati ya watu wazima 100 chini ya umri wa miaka 50 waliishi pamoja nje ya ndoa katika miaka ya sitini, hii imeongezeka hadi 1 kati ya 5 leo (ONS), ikiwa ni familia milioni 3.3 (ONS). Ukweli ni, kuishi pamoja huku nje ya ndoa ni aina ya familia inayokuwa kwa kasi kwa zaidi ya miongo miwili nchini humo. Hii ni licha ya ukweli kuwa ripoti baada ya ripoti, utafiti baada ya utafiti zimefichua kuwa ndoa ndio njia imara zaidi pekee ya kulea watoto, huku kukiwa na uwezekano mkubwa wa familia zilioundwa kwa kuishi pamoja nje ya

ndoa kushuhudia kutengana kwa wazazi wao kabla ya umri wa miaka 12 ikilinganishwa na watoto waliozaliwa na wazazi waliooana.

Kama natija ya muondoko huu huru wa kimaisha katika Magharibi, hivyo basi haishangazi kuwa uzazi wa watoto nje ya ndoa umeongezeka pakubwa ndani ya dola hizi. Tarakimu za Eurostat zaeleza kuwa kiwango cha watoto waliozaliwa hai nje ya ndoa katika nchi 28 za EU mnamo 2014 ilikuwa ni asilimia 42. Mnamo 2015, idadi ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa iliipiku idadi ya watoto waliozaliwa ndani ya ndoa katika dola nyingi wanachama wa EU: Ufaransa – asilimia 59, Sweden – asilimia 55, Denmark – asilimia 56, Estonia na Slovenia (asilimia 58) (Eurostat). Nchini Uingereza, takriban nusu (asilimia 47) ya watoto huzaliwa nje ya ndoa (ONS), huku katika miaka ya arubaini ilikuwa karibu asilimia 6. Kwa mujibu wa utafiti wa wasomi katika Chuo Kikuu cha Amerika cha John Hopkins, uliochapishwa mnamo 2012, asilimia 57 ya wazazi nchini Amerika walio na umri kati ya miaka 26 na 31 wanapata watoto nje ya ndoa.

Kuongezea tsunami hii ya kuvunjika kwa familia katika Magharibi, vile vile kuna matatizo mengine makubwa yanayoathiri maisha ya familia, kama vile wazazi kukosa muda wa kukaa na watoto kutokana na kuwa wazazi wote wawili baba na mama wamebanwa na matarajio ya kikazi ambapo pia yanadhuru ndoa; mateso ya “mwanamke bomba” kung’ang’ana ili kuweka mizani sawa kati ya majukumu ya kinyumbani na kudumisha taaluma au kazi; na kupunguza kiungo cha familia kwa wanandoa kuchagua kuwa na watoto wachache au hata kutokuwa na watoto kabisa imesababisha upungufu wa ‘watoto’ katika nchi kadhaa ikiwemo Ufaransa, Ujerumani na Uhispania, ikipelekea kuwepo kwa idadi kubwa ya wazee na vijana wachache wa kuwaangalia wazee hao.

Kuporomoka kwa thamani ya maisha ya familia nchini Uingereza na mujtamaa nyengine nyingi za kisekula za Kimagharibi ni dhahiri kuona, kama zilivyo natija za familia kuvunjika au kukosa maelewano ambayo imeathiri vibaya maisha ya wengi, hususan watoto na kupanda mbegu za mrundo wa matatizo ya kijamii kwa dola hizi. Hakimu Paul Coleridge alielezea kuwa kuzidi kwa kiwango hiki cha juu cha kuvunjika kwa familia nchini Uingereza ni kama, “... tamasha lisilo na mwisho la mateso ya mwanadamu. Mto usio kauka wa machungu ya mwanadamu”.

Sehemu ya 2 ya makala haya itatathmini sababu msingi za kuyeyuka kwa familia katika dola huru za kisekula za Kimagharibi.

Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

**Dkt Nazreen Nawaz
Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

“Kuyeyuka kwa Familia” za Mujatamaa wa Kisekula wa Kimagharibi

SEHEMU 2: Sababu za Kuyeyuka kwa Familia Katika Dola za Kisekula za Kimagharibi

Serikali za Kimagharibi zimejaribu kuzindua miradi kadha wa kadha ili kuzuia wimbi la kuvunjika kwa familia ndani ya mujtamaa zao. Lakini, haya yameambulia patupu. Hii ni kwa sababu wameshindwa kutambua kwamba sababu msingi za kuyeyuka huku kwa familia ni maadili msingi ya kisekula na ukosefu jumla wa umuhimu unaopatiwa ndoa na maisha ya familia ndani mujtamaa huru za kirasilimali.

Uhuru Uso Mipaka wa Kibinafsi na Kingono:

“Uhuru wa kibinafsi na kingono” juu ya msingi wa mujtamaa huru umekuza dhana ya ubinafsi na kutojali chochote maishani kwa msingi wa utafutaji matamanio na matakwa ya kihayawani kuliko kukuza fikra ya kuhisabiwa katika vitendo vya mtu na uwajibikaji juu ya wengine. Imesababisha watu wengi kuchukua ndoa kutokana na hofu juu ya kujitolea, uaminifu na majukumu yanayohitajika – kuitazama ndoa kama “kizuizi cha uhuru wao” na badala yake kufadhilisha “uhuru na useja” na kuwa na mahusiano ya kijinsia na “yeyote, wakati wowote”. Imebua utamaduni wa uzinzi unaopelekea viwango vya juu vya mimba za matineja nje ya ndoa, uavyaji mimba, kina mama wapweke na zinaa ambayo ni moja ya sababu kuu za talaka katika mujtamaa nyingi huru. Kwa mujibu wa utafiti ulionukuliwa na gazeti la ‘The Independent’, asilimia 50 hadi 60 ya wanaume waliooa na asilimia 45 hadi 55 ya wanawake walioolewa nchini Uingereza hufanya zinaa. Kwa mujibu wa tarakimu kutoka gazeti la ‘The Times’, zinaa inajumlisha asilimia 12 ya sababu za talaka nchini Uingereza. Abigail Lowther, wakili aliye na kampuni inayohusika na sheria ya familia, alisema kuwa ukosefu wa uaminifu nchini Uingereza ulikuwa “ukiongezeka kwa kasi” ikilinganishwa na aina nyenginezo ya tabia zinazohusishwa na talaka. Nchini Denmark, asilimia 46 ya wanandoa washawahi kuwa na uhusiano kwa mujibu wa idadi kutoka Statista. Na nchini Amerika, baadhi ya tafiti ziligundua kuwa 1 katika ya watu 3 alikiri kumdanganya mwanandoa mwenzake. Ukweli ni, ndani ya mujtamaa huru, utukufu wa ndoa na uaminifu umemomonyoka kiasi ya kuwa biashara zinazotoa ‘huduma za zinaa’ zinaendeshwa kihalali ndani ya dola! Lakini, falsafa ya kupata upeo wa juu wa uhuru wa kibinafsi haiwapi watu furaha ambayo kimsingi watu wanahitaji. Ripoti ya shirika la Msalaba Mwekundu la Uingereza na Ushirika, iliyo chapishwa mnamo Disemba 2016, iligundua kuwa talaka na kuvunjika kwa familia imepelekea janga la upweke nchini Uingereza. Ukweli ni, imewaacha Waingereza milioni 9 na upweke.

Utamaduni na muondoko huu wa uhuru wa kimaisha yamesababisha pia hali ambapo mtu huenda akawa na mahusiano nje ya ndoa na idadi kadhaa ya wanawake na kuwa baba wa watoto kutoka kwa kina mama tofauti tofauti, huku akikosa kuchukua jukumu lolote la kimwili au la kihisia la mtoto wake au mamake isipokuwa tu uwezekano wa malipo ya hundi moja tu kila mwezi. Hii imeyatishia maisha ya mamiloni ya watoto na wanawake. Hakimu Paul Coleridge, aliyekuwa jaji wa Mahakama Kuu ya Uingereza katika kitengo cha familia, alieleza kuwa hali hii ni kama, “mchezo uso kwisha wa ‘mahusiano ya kimuziki’ au ‘pitisha mpenzi’, ambao sehemu kubwa ya watu wanajihusisha nao ... kiu iso mwisho na yenye kuambulia patupu ya kutafuta uhusiano imara.” Ni hali ambayo pia imesababisha ukosefu wa uaminifu katika watu wanaotafuta wenza katika ndoa, kwa kuwa hawana hakika kama uhusiano huo umejengwa juu ya utiifu, uaminifu na uangalifu au la, na wana wasiwasi kuhusiana na kuweza kudumu katika mazingira kama haya yaliyojaa uzinifu na kujistarehesha binafsi. Ni mojawapo ya sababu za kushuka kwa viwango vya ndoa kwa wamagharibi huru.

Fauka ya hayo, fikra hatari iliyo kuzwa na maadili huru yanayo shajiisha watu kufuatilia na kutenda kwa mujibu wa matamanio na matakwa yao, sambamba na kuwadunisha wanawake ndani ya mujtamaa huru zinazo idhinisha ngono na kuiweka kama lengo katika sekta tofauti tofauti, ni jambo linalochangia pakubwa janga la ghasia za kinyumbani zinazo ziathiri mujtamaa za Kimagharibi. Mmoja kati ya wanawake watatu ashawahi kuripoti baadhi ya aina za dhulma za kimwili au kijinsia tangu umri wa miaka 15 (Shirika la Umoja wa Ulaya la Haki Msingi (European Union Agency for Fundamental Rights)). Nchini Uingereza, mmoja kati ya wanawake wanne amepitia ghasia za kinyumbani katika maisha yake, na wanawake 2 huuliwa kila wiki na mpenzi wa sasa au wa zamani (Afisi ya Uingereza ya Takwimu za Kitaifa (UK Office for National Statistics)). Nchini Amerika, mwanamke mmoja hupigwa na mumewe au mpenziwe kila sekunde 15 (Shirika la Kitaifa la Uchunguzi (Federal Bureau of Investigation)) na watatu huuliwa na wapenzi wao kila siku (Muungano wa Kiakili wa Marekani (American Psychology Association)). Na nchini Australia, kila masaa 3 mwanamke hupelekwa hospitali kutokana na ghasia za kinyumbani (Kitengo cha Utafiti cha Masomo ya Jeraha, Chuo Kikuu cha Flinders (Research Centre for Injury Studies, Flinders University, Australia)).

Ubinafsi:

“Saratani” ya fikra ya ubinafsi ya “Mimi na nafsi yangu”, inayo kuzwa ndani ya mujtamaa za kirasilimali inayo tukuza kutafuta maslahi ya mtu binafsi juu ya kila kitu chengine imeila misingi ya muundo wa familia. Imesababisha watu binafsi kuangazia juu ya kile ambacho ni bora kwao kuliko kile ambacho ni bora kwa wanandoa wenza au ndoa, inayopelekea ongezeko la talaka. Imesababisha kuweka matamano yao juu ya hali nzuri ya watoto wao na mujtamaa, na kutenganisha kujihusisha na vitendo vyao na miondoko yao ya kimaisha na athari angamivu iliyoko kwa wengine. Imechangia watu kuchelewesha au kukataa kuwa na watoto hadi baadaye maishani ili kuyatumia vilivyo maisha yao ya kijamii, fedha za kibinafsi na uhuru wa kibinafsi. Kwa mujibu wa Afisi ya Uingereza ya Takwimu za Kitaifa (ONS), kiwango cha watoto waliozaliwa na wanawake walio chini ya miaka 25 nchini Uingereza na Wales kilishuka kwa asilimia 47 mnamo 1971 hadi asilimia 25 mnamo 2008. Ripoti ya ONS 2010 ya Miondoko ya Kijamii arubaini ilieleza kuwa idadi ya watu wanaoishi katika nyumba za familia na watoto ilishuka kutoka asilimia 52 mnamo 1961 hadi asilimia 36 mnamo 2009, huku idadi ya familia zenye mzazi mmoja zikiongezeka kutoka milioni 1.7 hadi milioni 7 katika kipindi hicho. Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni, wanawake katika umri wa miaka ya arubaini nchini Uingereza ni takriban mara mbili ya wale ambao kuna uwezekano wa kutokuwa na mtoto kama katika rika la wazazi wao, huku mmoja kati ya wanawake watano waliozaliwa mnamo 1969 akikosa kuwa na mtoto leo. Clare McNeil, mwandishi wa ‘Generation Strain’ (ripoti ya hivi majuzi kutoka katika Taasisi ya Utafiti wa Sera ya Umma) anaonya kwamba, “Idadi ya watu wenye umri kati ya 65 hadi 74 wasiokuwa na watoto wa kuwahudumia wakati wa uzeeni itaongezeka takriban maradufu kabla ya kumalizika muongo ujao,” na kwamba, “Kufikia 2030, zaidi ya watu milioni moja katika rika la umri huu hawatakuwa na watoto, ikilinganishwa na 580,000 mnamo 2012.” Sensa ya Amerika ya Taasisi ya Utafiti wa Watu iliyo chapishwa mnamo 2015 iligundua kuwa takriban (asilimia 47.6) ya wanawake nchini Amerika kati ya umri wa miaka miaka 15 na 44 hawajawahi kuwa na watoto. Inawakilisha asilimia kubwa ya wanawake wasiokuwa na watoto tangu taasisi hiyo ilipoanza kufuatilia takwimu hiyo mnamo 1976. Katika utafiti wa Amerika juu ya wanaume na wanawake wasiokuwa na watoto, kwa anwani: “Wawili wanatosha: Muongozo wa wanandoa wa chaguo la kuishi bila ya watoto” (Scotts, 2009) ulionukuliwa na ‘Psychology Today’ asilimia 80 ya walio shirikishwa, hususan wale walio chini ya miaka 40, waliiorodhesha kama yenye lengo imara taarifa - ‘Nathamini uhuru na kujiamulia’.

Ubinafsi umewasababisha wazazi kuwatelekeza watoto wao huku wakitafuta maslahi yao ya kibinafsi, na kuwasababisha watoto nao kuwatelekeza wazazi wao wakongwe, wakiwaona kama mizigo kwa wakati wao

na fedha zao binafsi, wakiwaweka katika nyumba za wazee ili wengine wawahudumie. Na kujali kibinafsi juu ya familia ya mtu (mke na watoto wake) na kutowatilia maanani au kuwatelekeza jamaa zake wengine, imesababisha ukosefu wa nidhamu ya usaidizi kwa familia kuu jumla inayokabiliwa na matatizo ya kimwili, kifedha na kihisia, ikiwafanya wengi kuteseka peke yao kimya kimya.

Usawa wa Kijinsia:

Ndani ya mujtamaa za kisekula za kirasilimali, kumekuweko na kudunishwa thamani cheo cha mama na maisha ya familia dhidi ya maisha ya kiuchumi. Katika ngazi ya kihistoria, mvutano wa Kimagharibi wa usawa wa kijinsia na kuibuka kwa utetezi wa wanawake iliyaweka maisha ya umma na dori asili ya mwanamume kuwa mtafutaji riziki juu ya maisha ya kibinafsi, cheo cha mama na dori asili ya mwanamke kuwa mjenzi wa nyuma. Watetezi wengi wa wanawake wana hoja kuwa heshima ya wanawake na uhuru hauko sambamba na kumtegemea mumewe kiuchumi au majukumu kamili ya kinyumbani, na hivyo basi, sio jambo tu la mwanamke kuwa na haki ya kufanya kazi bali kukaribia kuwa ni lazima kwa mwanamke kufanya kazi. Christabel Pankhurst, mtetezi mkuu maarufu wa wanawake na mwanachama wa harakati ya (kuwapigania wanawake wapewe haki ya kupiga kura) mwanzoni mwa karne ya 20, alisema kuhusu majukumu ya maisha ya nyumba kuwa ni mzigo usiovumilika juu ya wanawake walioolewa, upotezaji wakati na nguvu za kiuchumi, na hauna ujira wala hutambuliwi.

Leo, mojawapo ya natija za mtazamo huu wa maisha ya nyumba na fahamu ya “Usawa wa Kijinsia” ni kuundwa kwa mujtamaa ambazo wanawake sio tu wana haki ya kuajiriwa bali wanatarajiwa kufanya kazi hata kama ni kina mama wapewe walio na jukumu la kipekee la kuwachunga na kuwalea watoto wao. Fahamu ya usawa wa kijinsia ambayo nadharia yake ilikuwa kuzalisha “mwanamke mwenye kila kitu”, kiuhalisia ilizalisha “mwanamke mtendaji kila kitu” – aliye endelea kubeba mzigo wa majukumu ya mama na majukumu ya familia lakini sasa pia anang’ang’ana na mzigo zaidi wa kuimudu familia yake kifedha. Huku wazazi wote wawili wakiwa watafutaji riziki katika familia nyingi, kumekuweko na mvutano wa kudumu wa kutafuta muda kwa ajili ya watoto au muda wa kuziimarisha ndoa, aghalabu inayoleta mvutano katika uhusiano kati ya mume na mke. Hivyo basi, Usawa wa Kijinsia, ambapo mtu anaangalia kile ambacho ni bora kwa mwanamke kwa mkabala na kile ambacho ni bora kwa mwanamume kuliko kile ambacho ni bora kwa familia au jamii kupuuza kile ambacho ni bora kwa ajili ya kuimarisha ndoa kwa ajili ya watoto na kwa ajili ya mujtamaa kwa jumla. Fauka ya hayo, usawa wa kijinsia, unaomomonyoa kuridhia tofauti za kijinsia na dori, pia imeathiri utambuzi ndani makazini na katika mujtamaa wa umuhimu wa cheo cha mama, ikipelekea waajiri wengi kushindwa kuwajali vilivyo wale

Endelea Uk..10

JARIDA LA
UQAB

wanawake wenye watoto wadogo, kama kuwapa masaa muwafaka ya kazi au mahitaji mengineo yanayotakikana, wakipuuzilia mbali umuhimu wa majukumu yao katika familia zao.

Fikra ya kimada:

Nidhamu ya kimada ya kirasilimali, iliyoweka mbele utafutaji wa mali kama lengo lake kuu la kimfumo imefadhilisha faida juu ya watu na fedha juu ya familia. Imeanzamia kwa njia ya kudumu juu ya utafutaji rasilimali za serikali au mapato ya biashara juu ya uchungaji familia. Msukumo huu wa kudumu kwa ajili ya faida ya muda mfupi umedunisha cheo cha mama na maisha ya familia na kuwalazimisha hata kina mama wapweke kufanya kazi, ikiwaacha na muda mchache wa kulea watoto wao barabara. Hakika, aghalabu kuna vishajiisho vya kifedha vya kina mama kurudi kufanya kazi; vishajiisho vichache zaidi kwao kukaa nyumbani na kuhakikisha ulezi imara wa watoto wao. Kuthamini huku mada juu ya cheo cha mama kumepelekea hali ambapo mwanamke mja mzito au yule aliye na watoto wadogo aghalabu kuonekana kama mzigo kwa kampuni kuliko kuwa ni rasilimali kwa mujtamaa. Utafiti kwa mameneja 500 uliofanywa na kampuni ya sheria ya Kiingereza, Slater & Gordon ulio chapishwa mnamo 2014, unaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 40 walikiri kuwa kwa ujumla hofu ya kuajiri mwanamke aliyefikisha umri wa kuzaa, huku idadi kama hiyo hiyo wakiwa na hofu kuajiri mwanamke ambaye tayari ana mtoto au kuajiri mama katika cheo kikubwa. Thuluthi moja ya mameneja katika utafiti huu walisema kuwa ni heri waajiri mwanamume wa umri wa miaka ya ishirini au thalathini kuliko mwanamke wa umri huo huo kwa kuhofia wao kuchukua likizo ya uzazi. Utafiti wa 2005 kwa kampuni 98 nchini Uingereza wa Shirikisho la Uajiri uligundua kuwa 3/4 ya biashara ni heri zivunje sheria kuliko kumuajiri mwanamke mja mzito au aliyetimu umri wa kuzaa. Natija yake ni kuwa sio tu kuwa wanawake wanashinikizwa kuingia katika ajira na kutarajiwa kupokea mishahara kwa ajili ya familia zao, bali wanabaguliwa makazini kwa kuwa na uzao! Natija yake ni kuwa wanawake wengi wanafadhilisha kuchelewesha kupata watoto au kubaki bila ya watoto kuliko kukabiliana na “hukumu hii ya uwezo wa kuzaa” katika mapato yao au taaluma zao. Inaonekana kuwa, kwa wanawake wengi Magharibi, “kutiwa minyororo jikoni” kumebadilishwa kwa “kutiwa minyororo katika soko la kiuchumi”. Haya ni miongoni mwa mambo yanayochangia viwango vya chini vya uzazi na ‘mgogoro wa uwezo wa kuzaa’ yanayo athiri dola nyingi za kirasilimali za kimagharibi leo ambayo yana athari angamivu kwa mujtamaa, ikiwemo idadi chache ya watu wa kuwahudumia wazee. Mtu pia asisahau janga la kihisia wanalopitia wale wanawake wanao lazimishwa kufanya matibabu ya IVF ili kuzaa kutokana na kupungua kwa uwezo wa kuzaa, kupoteza mimba na kungezeka kwa matatizo ya ujauzito yanayo nasibishwa na kuchelewesha kuwa mama.

Tamati:

Ni dhahiri kuwa ni maadili na sheria za nidhamu huru ya kisekula ya kirasilimali zinazotekelezwa ndani ya dola nyingi za kimagharibi ndiyo shina la tatizo la ghasia na kuangamia kwa muundo wa familia ndani ya mujtamaa zao. Hakika, nidhamu hii kimaumbile imeundwa kusababisha ukosefu wa utulivu katika familia na kuvunjika kwake, ikisababisha mateso ya kibinadamu yasiyo elezeka kwa watu wengi mno na watoto na matatizo yasio na idadi kwa dola.

Lakusikitisha, Ummah wa Kiislamu unaoishi Magharibi au katika ulimwengu wa Kiislamu haujakingwa kutokana na maadili haya ya kisekula au ya kirasilimali kutokana na kuzama ndani ya mazingira na kuishi chini ya nidhamu zinazopigia debe na kushabikia maadili haya yasiyokuwa ya Kiislamu. Natija yake ni kuwa fahamu ya “ndoa imara” na “viungo vya familia imara” ambazo daima zimefahamika na Waislamu kwa vizazi vyote kuwa ndio kitovu au msingi wa jamii imara leo pia zimemomonyoka ndani ya Ummah wa Kiislamu. Kama Waislamu, ni muhimu mno tuchukue mafunzo kwa makini kutokana na kuyeyuka huku kwa muundo wa familia ambao umejitokeza ndani ya mujtamaa za kimagharibi na kupinga itikadi, maadili na nidhamu zilizo sababisha ghasia hizi za kijamii, ili jamii zetu zisifuate njia hiyo hiyo ya maangamivu. Hii ni pamoja na kufahamu waziwazi na kukumbatia maadili, sheria za kijamii na nidhamu sahihi ya Uislamu ambayo pekee ndiyo yaliyojijami ili kutatua matatizo mengi yanayo athiri utulivu na umoja wa maisha ya familia katika Ummah wetu.

“Katika miongo ijayo, mafanikio yatakusanyika tu kwa zile tamaduni zinazo hifadhi hadhi ya familia.” Joel Kotkin – Mwandishi wa ‘Watoto Wote Wamekwenda Wapi?’ na Msomi wa Masomo ya Mijini kutoka Chuo Kikuu cha Chapman eneo la Orange, California, Amerika.

Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

**Dkt. Nazreen Nawaz
Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake Katika
Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

Mama, Mke, na Mke Nyumbani: Malipo ya Utumwa wa Uzaaji Watoto! Hivi Ndivyo Namna Usekula Ulivyo Yafisidi Maisha ya Wanawake!

Nini maana ya mwanamke kuwa mama, mke na mke nyumbani kwa mujibu wa itikadi inayokataa maadili yote ya utu, akhlaqi, au ya kiroho kwa sababu inaona kuwa manufaa ndio kipimo cha vitendo na kwamba manufaa ndio mizani na kinacho pimwa? Itikadi hii huona kuwa wanadamu huthaminiwa kwa mujibu wa uzalishaji wao ndani ya mujtamaa na kwa kiwango cha mapato yao ya kimada! Hivyo basi, mke nyumbani si mmoja wa watu wanaozalisha kwa sababu hukmu inayo pimiwa watu ni: "Ikiwa mtu atafanya kazi atafanikiwa". Lakini mama na mke nyumbani wako nje ya mpangilio huu mpya wa kimataifa kwa sababu hawafanyi kazi ya kulipwa, na kwa sababu wamefungika na mume, watoto na familia kama ilivyotajwa katika waraka wa Beijing.

Ikiwa mwanamke anafanya kazi bila ya malipo au ujira; anafanya kazi kwa bidii na kuchoka na kujitolea wakati wake, afya na juhudi pasi na mapato ya kimada, inazingatiwa kuwa ni ujinga na kubakia nyuma ikiwa ni kwa ridhaa yake, au huonekana kuwa ukandamizaji na kukiuka haki zake ikiwa ni kwa kulazimishwa.

Hii ndiyo sababu wanawake kama kina mama, wake na wake nyumbani huorodheshwa ima kama wasiojitendea haki au kukandamizwa; ima walichagua kwa khiyari kuishi na jukumu duni la kiasili, kujiweka mbali na ushirikiano wa ujenzi na uimarishaji wa jamii zao, na kujimakinisha na kujenga uhuru wao. Na kwa kuwategemea wanaume kuwapa masrufu yao na uangalizi wao, wamekuwa mzigo kwa familia na wasiokuwa na maana. Uorodheshaji huu umewatia mtegoni wanawake katika machaguo yao, na kuwaweka katika hisabu na maswali endapo watalalamika au kudai haki zao zozote. Kwa vyovyote vile, sheria haiwalindi wajinga na wale waliojipuuza! Na kabla ya hilo, inawaanika wanawake kukejeliwa na hata kuchukiwa na wanawake wengine! Na huenda wakatelekezwa na waume zao ikiwa watabeba imani kuwa maisha ya ndoa ni ushirikiano katika dori na majukumu, na sio kuwa kila mmoja ana majukumu yake maalumu; kwa hiyo anakataa kuwa mtoaji masrufu wa pekee, na mwanamke awe mwenye kufaidika na mpatilizaji!

Kigawanyo cha pili hupokea maliwazo na uungwaji mkono kwa sababu mwanamke hakuchagua kujiweka katika sanduku hilo, bali ndoa, familia na watoto ni uovu usioepukika. Na hii ndiyo kadari nyeusi inayo wasubiri wanawake wenye kufeli, ambao hawakufanikiwa kimasomo! Mwanamke anapokea maoni haya yanayo muonesha yeye kama mwathiriwa, na rai kuwa lau angekuwa na kazi maishani, ni bora zaidi kuliko kufungwa katika kuta za nyumba, akisafisha, akipika na kulea watoto wake, na kwamba kazi yake ndani ya nyumba yake ni kumdunisha na kumnyima haki zake.

Swali la – "Kazi yako ni nini?" – linamtia hofu na kero, na aghalabu hujibu kwa haya na aibu: "Kwa bahati mbaya niko nyumbani!"

Wanawake ambao ni mfano wa kuridhika, heshima, cheo, kusafiri na walio ngangari. Ni wale wanaofanya kazi ili kujidhihirisha na kupambana na mipaka ya ghariza zao, na hawakubali kuwa bila ya ajira au kutengwa na dori yao kufungika tu kama "mashini ya kutengeza watoto" na kuangalia nyumba, na kushindana na wanaume wakati mwengine katika kazi nzito na ngumu. Wao huziepuka dori msingi zilizotayarishwa kwa ajili yao, na kuvunja vizuizi vya kuwategemea wanaume. Mwanamke huyu huenda akaolewa na kuzaa, lakini hasikizi uzushi juu ya mama na mke na ulezi wa watoto, bali anatia juhudi na nguvu zake maradufu kwa gharama yake na familia na watoto wake, ili asipoteze Medali ya Heshima inayopokewa na serikali, taasisi, vyombo vya habari na mashirika ya utetezi wa wanawake kwa kuwa mwanamke ngangari aliye na uwezo wa kukabiliana na changamoto hizi!! Lakini swali linabakia: Ni nani aliyeziweka changamoto hizi na masharti haya yasiyompa utu kamili isipokuwa anapo jinyongoa zaidi na kupuuza majukumu yake ya kighariza chini ya kisingizio cha kujinadi kibinafsi? Je, lengo nyuma yake ni kupata maslahi ya wanawake au maslahi ya warasilimali walafi?

Maoni yote haya yaliafikiana na maendeleo ya kiviwanda katika nchi za Kimagharibi, zilizoona haja ya wanawake kushiriki katika kazi nje ya nyumba na wanaume ili kuongeza uzalishaji. Na kwa kuwa nguvu kazi ni lazima iwe rahisi, wanawake ndiyo chaguo bora. Hata leo, mwanya wa ujira kati ya wanaume na wanawake unaweza kuonekana miongoni mwa wale wanaofanya kazi hizo hizo kama wanaume licha ya wito wa usawa na madai ya kuondoa tofauti na ubaguzi baina ya wanaume na wanawake! Huu ni usekula katika mikataba yake mibaya na michafu zaidi; huwanyanyasa wanawake kwa gharama ya cheo chao cha mama, familia na mazingira ya kimaumbile kupitia kunadi madai ya kirongo ili kuwadanganya wanawake!

Usekula ulikiuka ghariza ya mwanamke na kuvuruga maisha yake siku ile ulipo hujumu dori ya mama na kuifunga katika kuzaa pekee. Dori hiyo iliachiwa mayaya na wafanyikazi wa nyumbani. Dori ya kuchunga watoto kwa sasa sio tena ya mama pekee. Hata fikra ya mama anayezaa ilitupiliwa mbali na kubadilishwa kwa mama badali anaye kodisha uzao wake, ikimpa mama asili fursa ya kufanya kazi na kujionesha na kudumisha swiha na mwili wake!! Kwa hivyo fungamano pekee baina ya mama na mwanawe, uzio wa kitovu, lina badali ya kimada aliyopewa na serikali za kirasilimali eneo la Magharibi kwa njia rasmi na ya halali; na hivyo

kufuta ghariza ya kike kikamilifu, na kukiuka moja wapo ya msingi mikuu: kuwa mama mbebaji mtoto tumboni mwake!! Hii ilimfanya mtetezi wa wanawake kuwa na ujasiri na kulilaumu umbile la kike. Simon De Beauvoir aliandika katika kitabu chake kwa jina 'The Slavery of Childbearing', "Kuzaa huufunga uhuru wa wanawake, kihakika ni utumwa ambao ni lazima upigwe vita, na mzizi wa ukandamizaji wanawake ni majukumu yao kuwa wajawazito, uchungaji na ulezi wa watoto!"

Wamagharibi wameamua kudhoofisha kinga ya jamii ya Kiislamu kupitia uenezaji wa neno "ukombozi wa wanawake" kumaanisha kuwa mwanamke ni mtumwa ambaye ni sharti akombolewe na kwamba amepotea na anahitaji kuokolewa. Kikwazo pekee cha ukombozi wake ni wale wanaoupigia debe! Shambulizi dhidi ya fahamu ya "mama, mke na mke nyumbani" ni kali hadi neno mke likawa linasifia hali ya kijamii kinyume na maana ya kindani iliyobebwa na wanawake wa Kiislamu kuhusu mume, uhusiano wake naye, fahamu ya utifu na uhusiano mwema, heshima, ukaribu na huruma. Fahamu hizi msingi, ambazo zimefafanuliwa katika nususi za kisheria, zinawasilishwa kwa njia chafu katika runinga, na hukumbwa na chuki na istihizai, au kupitia baadhi ya wahubiri na darasa za kidini katika runinga na idhaa, kuongeza chumvi sifa hizo ili kutuonyesha kuwa mke mwema ni kiumbe cha kindoto na sio mwanadamu wa kawaida.

Filamu, musalsala, hadithi na riwaya zimeunda sura mpya kwa mwanamke wa Kiislamu kuhusu ndoa kama fungamano la kimasharti lililojengwa juu ya usawa wa haki na majukumu, kuheshimu uhuru, haki ya upinzani, ubadilishanaji majukumu ya kifamilia, uhuru wa kifedha na fahamu nyenginezo fisidifu zilizo potoka kutokana na ufahamu wa kisheria juu ya ndoa na mume. Na kuigeuza uwanja wa mzozo katika ushindani uliozushwa ambao ndani yake mwanamke ni lazima athibitishie thamani na ubwana wake; vyenginevyo, ataishia kuwa kama mke anayemsubiri mumewe jioni amletee unga aoke!

Serikali katika biladi zetu za Kiislamu zimetilia nguvu fahamu hizo potofu kupitia kupitisha kanuni kinyume na ufahamu wa kisheria. Kanuni kama hizo zinaamrisha kutoka kwa Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Dunia na taasisi zenye nguvu zinazofanya makongamano na warsha, yanayotoa maamuzi kuwa wanawake wa Kiislamu wamekandamizwa majumbani mwao chini ya usimamizi wa waume zao na kulingania kuachana na mila na destruri zinazotilia nguvu fikra hii. Makubaliano ya CEDAW hukadiria kuwa aina za ubaguzi dhidi ya wanawake huanza kwa kuzifunga dori zao kwa cheo cha mama, ndoa na ulezi, na hivyo basi, vifungu vilivyotiwa saine na biladi nyingi za kiarabu vimekuwa vya kuondoa aina za unyanyasaji kwa kuifanya ndoa ya mapema kuwa uhalifu, kupeana haki ya uavyaji mimba na talaka ... na hivi majuzi ni nchini Tunisia, ambapo ni haki kwa wanawake wa Kiislamu kuolewa na mwanamume kafiri!!

Hadhi ya mke nyumbani imetelekezwa na kuchukiwa, na hata katika kadi za vitambulisho rasmi katika nchi nyingi, sehemu ya taaluma inajazwa kama "asiye na ajira". Imeshuka hata kumwita "asiye na taaluma" katika baadhi ya nchi zinazodai kuwa viongozi wa haki za wanawake!! Lakusikitisha, dori ya mke nyumbani imekejeliwa na kutoheshimiwa sana katika biladi zetu za Kiislamu. Kazi imekuwa ni lazima na sio kwa mujibu wa haja ya wanawake kwake au haja ya jamii kwa kazi yake. Zaidi ya hayo, kazi hiyo haistahili maumbile ya wanawake. Janga kubwa ni kuwa kazi imekuwa ni shinikizo la kiuchumi linaloikamua nguvu ya mwanamke na kutumia masharti ya kimada yanayo dorora, kumnyima dori yake asili kama mama mchungaji wa watoto wake, mke mchungaji wa mumewe na mke nyumbani mchungaji wa nyumba yake pasi na kufikiria kuhusu udharura wa utafutaji riziki na kuhakikisha maisha ya sawa ambayo mume ameshindwa kupeana, au sahihi zaidi ni dola kushindwa kupeana!

Matokeo yake yakawa ni majanga; kutelekezwa kwa familia kukaenea ndani ya familia nyingi, na matatizo ya kindoa yakawa mengi kutokana na majukumu mazito na shinikizo za kimwili na kisaikolojia zinazo wazunguka wanandoa. Viwango vya utundu miongoni mwa watoto vimeongezeka kwa kutoweka kwa walezi wao katika ufuatilizaji na uangalizi. Familia nyingi zimevunjika na viwango vya talaka, viwango vya useja na kuzembea katika kuoa na kuvunjika kwa mkataba vimeongezeka!!

Kwa kuwa taasisi ya familia ni msururu wa duara zilizounganika pamoja, imeundwa na kulindwa na sheria ya Allah. Wamagharibi wametambua umuhimu wa dori ya wanawake katika taasisi hii na hivyo kuwalenga kama kina mama, wake na wake nyumbani katika jaribio la kuzalisha sura ya wanawake wa Kimagharibi katika muundo tatanishi mno!

Lakini ni jambo lisiloweza kukataliwa kuwa orodha ya vipaumbele vya wanawake wa Kiislamu imegeuka juu chini. Dori ya mama, mke na mke nyumbani sio tena mishi yao ya kwanza. Dori kubwa na ujira wa mama kwa Allah (swt) imepotea isipokuwa yeye (mama) atekeleze dori yake vyema, amche Allah na ajali na kuwajibika katika nyumba yake. Uislamu umedhamini maisha thabiti na ya utulivu kwa wanawake kama wanadamu, ukizingatia ghariza yao na kuwapa majukumu katika njia inayo kwenda sambamba na mazingira na maumbile yao. Inabakia kusemwa kuwa utekelezaji wa hukmu hizi za kiwahyi ni jukumu la kisheria kwa wanaume na wanawake na hukmu hizi ni lazima zitekelezwe na dola inayounda mazingira muafaka kwa wanaume, wanawake na familia.

Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

Nisreen Budhafri

Familia ya Kiislamu ... Na Hatari za Kuvunjika



Familia ya Kiislamu imepigwa na hatari kubwa sana inayoitishia kutoweka, kuvunjika misingi yake na kutahadharisha maangamivu yake na kukata mafungamano ya jamaa zake. Kiungo cha familia, kilicho tawaliwa na mapenzi, mshikamano na utulivu, kiinje inaonekana kuwepo na umoja, lakini kindani imegawanyika, imeunganishwa tu na kuta za nyumba au meza ya chakula; nyumba ambamo mtu anaishi kama ambaye hajulikani miongoni mwa wengine na hawashirikishi katika hofu na matatizo yake binafsi! Kuvunjika huku kumewakumba wanafamilia na kuwapasua na kuwafanya waishi kibinafsi binafsi, wakiteseka kutokana na natija ya mfarakano, upweke, huzuni na kupoteza.

Kiungo cha familia – taasisi ya kwanza kuu yenye kumlea mtoto na kumjenga fahamu ili kuzitekeleza maishani mwake na kuunda shakhsiyya (utambulisho) yake – iliathiriwa na mambo mengi yanayo lihujumu umbile lake. Hivyo basi, dori za familia zildunishwa na matatizo mengi yakaibuka; ilitawaliwa na ukavu na mafungamano ya mapenzi yakavunjika na kila mwanafamilia akawa na ulimwengu wake kivyake. Watoto hawawazingatii wazazi wao au ushauri wao: utundu na uchoyo umetawala; hawaoni kupuuza haki za wazazi kama dhambi au kosa. Wazazi pia wanashiriki katika lawama hii ya hali ya watoto wao kwa sababu ya kutofanya kazi yao ya kuwalea watoto kwa umakinifu.

Maradhi mabaya yanayoisibu familia ya Kiislamu yanayoitwa “kuvunjika kwa familia” ndio tatizo kuu sawia na matatizo mengi yanayoukumba Ummah wa Kiislamu. Ni nini iliyo yasababisha? Je, yatatibiwa vipi?

Kuvunjika kwa familia ni kuyeyuka kwa mafungamano ya familia na kudhoofika na kutoweka kwa mapenzi miongoni mwa wanafamilia huku uhusiano wao unapo kauka; mapenzi sio sehemu yake tena, na nyumba hugeuka kuwa “bweni” ambamo wanafamilia huishi tu na kula humo. Mwanza mkubwa uliundwa kati ya wanafamilia na kila mmoja wao anaishi kama mgeni kwa mwengine. Ni hatari sana huku kuyeyuka kwa mvunjiko wa familia ni mvunjiko kwa mujtamaa na Ummah wa Kiislamu ulioipatia familia umuhimu mkubwa kama Dini yake ilivyo fundisha hili, na kufafanua kuwa hali nzuri na amani katika mujtamaa imefungamanishwa na kiungo cha familia.

Allah (swt) amesema:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً
وَرَحْمَةً

“Na katika alama zake ni kule kukuumbieni kutokana na nafsi zenu wake ili mupate utulivu ndani yao; na akajaaliya baina yenu mapenzi na huruma. Hakika katika hilo zimo dalili kwa watu wenye kutafakari” [Ar-Rum: 21].

Nyumba ni mahali pa utulivu na ustawi.

Huwafungamanisha wanachama wake kwa mapenzi na huruma, na huunganishwa kwa elimu na hukmu za Uislamu; hushindana katika matendo mema ili kupata ujira wake. Baba huchunga familia yake na mama humtii mumewe na kumridhisha na kuwalea watoto wake na kuwazunguka kwa mapenzi na upole. Kila mmoja wao anajua haki za mwenzake na kutafuta jinsi ya kuzitimiza ili kupata radhi za Allah. Uislamu hukuza fahamu kuu zinazotilia nguvu mafungamano ya familia na kuyafanya kuwa ya kipekee. Uislamu ulizitambulisha dori na kumpa kila mwanafamilia kazi ya kusaidiana wenyewe kwa wenyewe ili meli hiyo (kiungo cha familia) isafiri pasi na misukosuko ya upepo au dhoruba, ikiongozwa na nahodha anaye saidiwa na wasaidizi. Kila mmoja wao anatekeleza dori aliyopewa ili kufika salama: radhi za Allah na kuingia katika Pepo Yake.

Uhusiano kati ya wanaume na wanawake ni uhusiano wa amani, utangamano na utulivu. Sio uhusiano wa vita ambapo uhasama, mizozo na uadui umetawala. Kila upande unajua kazi yake na wanasaidiana wenyewe kwa wenyewe. Katika Malalamishi yake kwa Mtume (saw) kuhusu mumewe, Khawla alisema, “Ewe Mtume wa Allah, nikiwatelekeza watoto wangu watapotea na ikiwa nitawaangalia watakabiliwa na njaa...” Utambuzi na ufahamu huu wa dori unafanuliwa waziwazi na Khawla Allah awe radhi naye. Anajua kwa yakini kuwa jukumu lake ni kuwalea watoto wake na jukumu la baba ni kuwaangalia kimasurufu; wote wanasaidiana na kuwalea watoto kisahihhi pasi na ukatili au kuwadekeza zaidi ili mtoto asikulie kwa chuki na ukosefu wa fadhila au dhaifu na mwepesi wa kukosa heshima kwa wazazi au kutowaangalia.

Mtume (saw) asema: «كفى بالمرء إثماً أن يضيع من يقوت» Yatosheliza kuwa ni dhambi kubwa kwa mtu kupuuzwa kutoa (Nafaqa) kwa wale ambao ni jukumu lake (mke, watoto, watumishi, nk).”

Wazazi wengi wametupa nyumba zao na watoto. Hakuna hisia za kiikhilasi na hakuna mapenzi wala upole!! Jukumu kubwa la wazazi limekuwa ni kutoa chakula na mavazi na vyombo za kisasa katika ulimwengu wa elektroniki katika tarakilishi, tablet na simu za rununu. Wako kwa ajili ya kuwapa watoto starehe lakini hawako maishani mwao; hawaonyeshi mapenzi, upole na hamu kwao; hawana muda wa kuzungumza nao na kukaa na kuwasikiza; kila mmoja yu mbioni akimbizana na wakati kufanya kazi nyingi isipokuwa kufikiria na kufanya kazi kwa bidii ili kuhifadhi umoja wa familia!!

Sababu nyingi zimepelekea kupasuka na kuvunjika kwa familia. Manung'uniko ya mara kwa mara yanayo endelea kati ya wazazi kutokana na mashindano ya kuendesha mambo ya familia na kugeuza dori za kimaumbile ambazo Allah ameziumba kwao husababisha mazingira ya msongo wa mawazo na hili huleta taharuki na kuteseka kwa watoto ndani ya nyumba, ikiigeuza nyumba kuwa mahali pa kuogofya na kutisha

palipo tawaliwa na chuki na uchoyo baada ya kuwa ni “chimbuko la utulivu, usalama, mapenzi na upole,” na mahusiano yamebadilika na kuwa tofauti nyingi ambazo wakati mwingine hupelekea talaka na kutengana kwa wazazi. Dkt. Seth Meyers, mwanasaikolojia wa Kiamerika na mtafiti katika mahusiano ya kijamii, anabeba mtazamo kuwa familia zinazo pitia taharuki na ugumu katika ulezi wa watoto aghlabu hukosa usaidizi wa kihisia na kijamii utotoni mwao, ima kwa kupuuzwa na wazazi wao au kutokana na kulelewa katika mazingira ya kifamilia yaliyojaa matatizo na ghadhabu, huku baadhi ya wazazi wakikabiliwa na tatizo kubwa na changamoto katika kumlea mtoto mtundu. Hii ndiyo siri ya uchungu wanaokabilia na. (Nahi As-Sarraf: malezi ya watoto ... Hisia kimya ya uchungu na hofu ya kufeli: Waarabu)

Tunapaza sauti za ving'ora juu ya viwango vya talaka katika familia za Kiislamu, ambazo zimeongezeka maradufu na kukua zikionya kuporomoka kwa kiungo hiki muhimu katika mujtamaa. Kwa mujibu wa tovuti ya “Aswat Magharibiya”, kesi za talaka katika eneo la Maghreb zimeongezeka katika kipindi cha miaka 8 iliyopita, na takwimu kunakili kuwa katika kila saa moja kesi 10 za talaka zinatokea, yaani kesi elfu 90 kwa mwaka, nchini Tunisia, kesi 41 za talaka zilinakiliwa kila siku, zaidi ya kesi 3 kwa saa moja, kwa mujibu wa “Habari za Al-Sabah” kutoka katika Wizara ya Haki. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Kituo cha Kiarabu cha Usajili na Takwimu, kesi sita za talaka husajiliwa kila saa moja nchini Algeria, iliyo wapelekea wachunguzi na wanaharakati wengi nchini Algeria kuonya kuenea kwa kadhia ya talaka nchini humo (euronews). Hali hii ni sawa na nchini Misri, ambayo ni ya kwanza duniani katika kiwango cha talaka; cha kesi 250 kwa siku ... wanandoa hutengana baada ya masaa tu ya kuoana ... wanawake milioni nne waliotalikiwa na watoto milioni 9 ni waathiriwa wa kutengana. (Al-Youm As-Sabi': 05/09/2017).

Morocco imeorodheshwa ya tano katika ulimwengu wa Kiarabu katika kiwango cha talaka ... kesi 5 za talaka hunakiliwa kila saa moja. Chini ya anwani: “Talaka nchini Libya, Kiwango cha Kutisha, na Nambari Zisizokuweko,” idhaa ya 218 ilisema kuwa makundi ya haki za kibinadamu yanasema kuwa kiwango cha talaka kimeongezeka pakubwa kwa zaidi ya miaka michache iliyopita. Ukadiriaji usiokuwa rasmi unadokeza kuwa kiwango cha talaka katika miaka ya hivi karibuni kimeongezeka hadi karibu asilimia 30, ambayo katika lugha ya nambari yamaanisha kuwa katika kila ndoa 100, kesi 30 zinafikia “mwisho wa furaha”.

N Post imethibitisha kuwa Kuwait imechukua usukani katika ongezeko la idadi ya talaka. Kwa mujibu wa takwimu, asilimia 60 ya mahusiano ya ndoa yalimalizika kwa kutengana katika sehemu ya kwanza ya 2017. Sheria ya Kuwait inawapa wanawake waliotalikiwa wa Kuwait idadi ya manufaa, ikiwemo mshahara wa kila mwezi, nyumba, gari na msaidizi. Hili ndilo linalo wapelekea baadhi ya wanawake kukimbilia kutafuta

talaka ili kupata huduma hizi (kwa mujibu wa Wizara ya Haki nchini Kuwait, kwa mujibu wa tovuti ya Arab Times Online Website). Mnamo 2016, idadi ya mikataba ya ndoa nchini Saudi Arabia ilifikia 157,000. Kinyume chake, kesi 46,000 za talaka zilitokea, yaani asilimia 30 ya uhusiano wa wanandoa humalizikia kwa kutengana. Nchini Uturuki, Idara Jumla ya Takwimu za Rekodi za Mahakama ilitangaza kuwa kesi za talaka katika kipindi cha miaka 10 iliyopita zilikuwa ni asilimia 82. Kesi za talaka jijini Istanbul zilikuwa ni asilimia 62.3 ya faili zote za kesi za kijamii mnamo 2016. (Al Ain News). Pakistan pia imesibiwa na maradhi haya ya kuvunjika na mauwaji ya heshima kuenea pakubwa. Tume moja ya Haki za Kibinadamu imenakili mauwaji 280 chini ya kisingizio cha heshima kuanzia 2016 mpaka Juni 2017.

Ama kuhusu sababu zake, ni kutokana na haswa na uhuru wa kujitegemea kimada kwa wanawake na kuegemea fahamu za uhuru kutokana na mamlaka ya wanaume na uwezekano wa kuachana naye, hususan ikiwa mwanamke hana furaha na mumewe au ikiwa kuna dosari ya awali katika uhusiano inayopelekea matatizo ya kimada yanayo chochea mfadhaiko wa kisaikolojia baina ya wanandoa, inayopelekea taharuki katika uhusiano wa kihisia kutokana na kushinda kuyamudu mahitaji ya kimada ya familia.

Na viwango hivi vya juu vya kuogofya sio vyote bali ni mifano tu; nchi nyingi nyenginezo zinaugua kutokana na kadhia hii inayo enea na kuenea katika familia za Kiislamu kwa sababu ziko mbali na fahamu sahihi za Kiislamu za ndoa ambayo ni mkataba mzito ulio waunganisha wanandoa, na talaka zinatokea kwa sababu ndogo ndogo ... Matatizo mengi makubwa mara nyingi hupelekea talaka na kuporomoka kwa familia na hali nguvu kwa watoto.

Kama natija ya kuvunjika huku na kufarakana, wanafamilia huhisi kupotea na kuishi pasi na usalama; ni wanyonge na kushindwa kutatua matatizo inayo wapelekea kutafuta njia rahisi zaidi na za karibu, hata kama si za halali na kuwaletea hasara.

Kwa kuwa wanajua umuhimu mkubwa wa familia ya Kiislamu ni kujenga watoto na kuwatayarisha kuwa wanaume wa mustakbali, Wamagharibi wametumia mbinu na njia zote kueneza sumu yao ili kuivunja na kuimaliza. Wametulizia makini juhudi zao kwa wanawake, walio na jukumu la ulezi wa vizazi, na kuamua kuchafua na kufisidi fahamu zake sahihi kwa fahamu zao fisidifu zinazomfanya kutupa dori yake muhimu zaidi ambayo Allah alimchagulia yaani, ulezi wa watoto na kuwajenga. "Mama ni shule, ukimuandaa, unawaandaa watu wenye suluki nzuri." Wamagharibi wamebuni majukwaa na kufanya makongamano na warsha ili kueneza fikra huru za uharibifu. Catherine Forth, Profesa wa Kiamerika, alisema, "Makongamano na makubaliano ya kimataifa yanayohusu wanawake, familia na watu ... kwa sasa yanaundwa ndani ya

mashirika na kamati zinazo tawaliwa na mambo matatu: utetezi mkali wa wanawake, kupambana na ongezeko la uzazi na watu, mahusiano ya kimapenzi baina ya jinsia moja kwa wanawake na wanaume. Kamati ya wanawake katika Umoja wa Mataifa ilianzishwa na mwanamke wa Kiskandinavia anaye amini ndoa ya wazi, kupinga familia, akikadiria kuwa ndoa ni kizingiti na kuamini kuwa uhuru wa kibinafsi ni lazima uwe wa kikamilifu ... Fahamu hii ya uhuru imeangaziwa katika kanuni zilizotolewa na kamati hii. Kutiwa saina kwa makubaliano ya CEDAW kunafanya kupinga ushoga – hata kwa kuchora vinyago – kitendo kinachompelekea mtendaji wake kuhisabiwa na sheria kutokana na kuwa "kinapinga haki za kibinadamu".

Hivi ndivyo Wamagharibi, ambao wataridhika pekee pindi Ummah wa Kiislamu unapofuata mfumo wao wa kimaisha, wanavyo taka. Wanapanga njama mchana na usiku kuhujumu hadhara yake na kuung'oa Ummah kutoka katika mizizi yake ya Kiislamu. Izza iko kwa Allah (swt). Atawashinda Wamagharibi hawa na kumaliza vitendo vyao na mipango yao, na Yeye (swt) atauregesha Ummah huu katika uongofu na kuupa ilhamu ya kurudi katika utawala wa baraka kwa sheria za Allah na kuasisi mujtamaa unaoongozwa kwa fahamu safi na za ikhlasi ambazo ndio msingi wa malezi ya watoto. Watakuwa ndio wale watakaolewa kisahih kwa mizani na kuwafanya taifa bora lililotolewa kwa watu.

Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

Zaina As-Samit

Mkono Mrefu wa Serikali Zinazotawala Katika Nchi za Waislamu ili Kuzifisidi na Kuzitia Usekula Familia!

Tunapozungumzia kuhusu familia, tunazungumzia kuhusu kiini kinachounda jamii, na hivyo basi, ufasidi wowote au dosari yoyote inayoathiri kiini hiki itaonekana katika jamii na dola nzima, achilia mbali kuzungumzia kuhusu mchakato wa mpangilio wa ufasidi wa kiini hiki, na vipi ikiwa ufasidi huu utafanywa chini ya masikio ya dola na macho yake, bali, ina mkono mrefu ndani yake, unaohisika katika nchi za Waislamu. Serikali zinazotawala hazikuacha juhudi yoyote katika kutia usekula na ufasidi ndani ya familia na mujtamaa wa Waislamu ili kuwaridhisha mabwana zao, Amerika na Ulaya, na ili kufikia hili wametumia viwango vikubwa vya pesa, na kufanya kazi kutekeleza hili kupitia mbinu kadha wa kadha, miongoni mwazo ni:

1. Utungaji na uingizaji kanuni na sheria kutoka ng'ambo zinazo kiuka vipengee vya Uislamu katika sehemu ile inayoitwa "Hadhi ya Kibinafsi": baada ya kuvunjwa Khilafah na kutoweka kwa Uislamu kama nidhamu ya utawala, vipengee vingi vilitoweka pamoja nayo kutoka katika uhalisia wa maisha, na Waislamu wakasalia pasi na sheria zozote zinazo tekelezwa kutoka katika dini yao wenyewe isipokuwa katika nyanja za ibada na kanuni za "Hadhi ya Kibinafsi". Lakini maadui wa Uislamu hawakuruhusu hata hizi pia kubakia, kwa hivyo walijaribu kuzitenganisha na maisha ya Waislamu. Kwa hivyo, waliunda vibaraka wao katika biladi za Kiislamu ili kutunga nidhamu ya kanuni na sheria kinyume na Uislamu na nidhamu yake ya kijamii, na kutabanni mtazamo wa Kimagharibi. Nchini Tunisia, kwa mfano, Bourguiba alitunga Kanuni ya Hadhi ya Kibinafsi mnamo 1956, ambayo alipotoka kutoka katika hukmu za kisheria na kudai kirongo kuwa haikukiuka sheria ya Kiislamu na kwamba imevuliwa kutoka katika roho yake na vipengee vyake japokuwa wingi wa kanuni zake imejengwa kutokana na sheria ya Ufaransa, na inajumuisha msururu wa kanuni ambazo ziko kinyume na hukmu za kisheria za kukatikiwa. Ambazo mifano yake ni mingi kama vile: kupuuza tofauti ya dini kama jambo linalokiuka ndoa kwa mujibu wa kanuni ya kimataifa ya haki za kibinadamu, inayosema kuwa "Wanaume na wanawake walio na umri uliotimu, pasi na mipaka yoyote ya kirangi, taifa au dini, wana haki ya kuoana na kuunda familia", na kama ilivyo marufuku ya ndoa ya wake wengi na adhabu kwa mume aliye na wake wengi kwa mujibu wa sura ya 18, kama vile ukiukaji wa hukmu ya Kiislamu iliyo tabanniwa. Na kisha wakaja wajukuu baada yake na kukamilisha mchezo wa ufasidi katika uwanja wa kijamii, na wakapambana na hukmu za Allah, utungaji wa kanuni kinyume na vipengee wazi vya Uislamu, ambapo kanuni mpya zilitungwa katika enzi ya El-Sebsi zinazo ruhusu ndoa ya mwanamke wa Kiislamu kwa mwanamume asiye Muislamu. Hivi majuzi, Raisi wa Tume ya Uhuru wa

Kibinafsi na Usawa, katika Afisi ya Raisi wa Jamhuri ya Tunisia, Bouchra Belhaj Hamida, alitangaza kuwa kamati imeanza kupendekeza kanuni itakayo jumuisha kumtaja mume pamoja na mke kama viongozi wa kisheria wa familia, kufutilia mbali mahari katika mkataba wa ndoa, ambapo aliikadiria kama matusi kwa wanawake, pamoja na kadhia ya usawa baina ya wanaume na wanawake katika urithi ambayo ndiyo inayobebwa kwa sasa.

Nchini Misri na Saudi Arabia, wanataka kuwekwa umri maalumu wa ndoa. Pia nchini Saudi Arabia, marekebisho yamefanywa kwa nidhamu ya usimamizi wa wanaume "Wilayah" juu ya wanawake, na mifano katika muktadha huu ni mingi, lakina hakuna nafasi ya kuitaja.

2. Amali na matukio ya kujiburudisha (sekta ya burudani): mipango ya burudani imekuwa miongoni mwa mbinu maarufu za kuingiza usekula na ufasidi katika familia za Waislamu. Haya yanajiri, chini ya kisingizio cha kuondoa shinikizo za maisha, kusaidia na kukuza vipaji, pamoja na kuzungumzia kuhusu kupata mapato ya kiuchumi na faida za kimada kwa ajili ya watu kutokana na miradi hii. Miradi na amali za ufasidi zinazo gongana na maadili ya Kiislamu na kupigia debe maadili ya Kimagharibi na kuyaingiza katika nchi za Waislamu. Wanatafuta njia ya kueneza uovu na uchafu miongoni mwa Waislamu, inayojumuisha mchanganyiko kati ya wanaume na wanawake na kufichua Awrah na maovu mengine chini ya guo la mamboleo na uwazi.

Saudi Arabia, kwa mfano, inayoshuhudia mpangilio wa kampeni ya kuibebesha umagharibi na usekula inayotekelezwa moja kwa moja na dola hiyo ili kuifurahisha Amerika, imetangaza mpango katika nyanja ya mabadiliko ya kiuchumi ya Kisaudi, ambao miongoni mwa nguzo zake ni sekta ya "Utamaduni na Burudani" na uwekezaji katika sekta ya utalii. Hivyo basi, kwa mujibu wa takwimu zilizotajwa, "Ruwaza ya Kitaifa" inalenga kuongeza maradufu matumizi ya familia katika utamaduni na burudani ndani ya Ufalme huo kuanzia asilimia 2.9 hadi asilimia 6. Katika muktadha huu, Mamlaka ya Burudani ilianzishwa kuambatana na Ruwaza ya 2030 iliyo wasilishwa na Mohammed bin Salman ili kihalalisha na kuidhinisha kisheria vitendo vyote vya ufasidi na muozo nchini Saudi Arabia. Kwa hayo, Haramu imekuwa Halali kupitia mashekhe wa Kisaudi baada ya miaka mingi ya ukandamizaji na upungufu, hususan kuhusiana na wanawake, na uovu (Munkar) ukawa wema (Ma'ruf) kupitia Mamlaka ya Burudani chini ya mwito wa uwazi. Kwa hivyo, iliandaa maonyesho, sherehe, na matamasha ya kisanii na muziki, na kusimamia kuanzishwa kwa sinema, ufunguzi wa Jumba la Opera, kuandaa mitindo ya wanawake, kuwaruhusu wanawake kuhudhuria mechi

Endelea Uk..17

za mpira, na kufanya matamasha ya mchanganyiko wa wanaume na wanawake.

Hafla na vipindi vingi pia zinaandaliwa katika biladi za Waislamu kwa usaidizi na udhinishwaji wa Dola hiyo ingawa haziandaliwi moja kwa moja nayo, kama vile vipindi vya vipaji (kucheza, kuimba na kuigiza) ambavyo vinapeperushwa na vyombo vya habari, pamoja na amali zilizoandaliwa na mashirika na taasisi zisizo za kiserikali.

3. Nidhamu ya kielimu na mtaala: fahamu ya familia na uhusiano kati ya wanachama wake imekumbwa na yale yaliyozikumba fahamu nyenginezo na fikra za ufisadi na kujaribu kuwatia usekula chini ya sera za kielimu ambayo haikujengwa juu ya Uislamu, na inatafuta kuiangamiza thaqafa ya Kiislamu katika nyoyo za watoto wa Kiislamu. Hii inaonekana waziwazi katika mabadiliko ya kudumu yanayofanywa na serikali tawala juu ya mtaala wa elimu kwa kuitikia maagizo ya mabwana zao, ambapo tunaamini kuwa marekebisha haya yanaangazia fahamu za haki za wanawake na usawa wao na wanaume, ambapo ni anwani pana ambapo hivi karibuni imebeba pamoja nayo miito kama utambuzi wa kibinafsi wa wanawake, kujimakinisha kibinafsi katika jamii na kuondoa udhibiti wa wanaume. Natija yake, elimu na utafutaji ajira zikawa ni kipaumbele kuliko ndoa na kuanzisha familia kwa wasichana wengi. Ndoa za mapema zilipigwa vita katika marekebisha haya ndani ya mipaka hii. Vilevile, miongoni mwa mada zilizohutubiwa zilikuwa ni afya ya uzazi kwa wanawake, haja ya mpango wa uzazi na kupunguza ukubwa wa familia na idadi ya wanafamilia. Ndani ya mpaka huu, tunawaona wakizigawanya familia kwa vigawanyo vya familia ya karibu (ndogo) familia pana (kubwa), wakizisifu familia za karibu na kuzikashifu familia pana, na kuzikadiria familia kubwa kama familia za “kitamaduni” huku familia zenye wanafamilia wachache kama “za kisasa”. Hii huonyeshwa katika sura wanazozitokea kwa ajili ya familia, hususan katika viwango msingi, ikilinganishwa na picha mbili, moja yapo ikiwa ni ya kale (picha ya familia pana) na nyengine ni ya kisasa (picha ya familia ndogo).

Baya zaidi, walibadilisha picha za kina mama na kina nyanya waliojifinika katika picha wanazo ziweka kwa ajili ya familia, pamoja na picha nyenginezo zinazo onyesha wanawake wakiwa hawakujifinika wakiwa na nguo za kimagharibi na mapambo, kama ilivyo katika mabadiliko ya hivi karibuni katika mtaala wa shule mnamo 2016 nchini Jordan na Palestina, pamoja na picha za wanaume ambao ndevu zao zimenyolewa zilizobadilisha picha za wanaume wenye ndevu. Katika njia hii iliyo fungamanishwa na akili za watoto hawa kuwa familia halisi ni familia ndogo, na kwamba kuyaona makosa haramu na kufichua uchi (Awrah) katika familia yao ni jambo la kawaida; bali, ni kuendelea kwa miji!

Katika muktadha wa watoto, haki za watoto na uhuru wa kuchagua vitendo vyake yamesisitizwa, na hata kama wazazi wanataka kuwazuia watoto wao kutokana na

kufanya jambo, au ikiwa watakumbwa na ghasia kutoka kwao, wanaweza kuishia polisi au mashirika ya haki za kibinadamu. Huu ni mwaliko kwa watoto kuwaasi wazazi wao, na ni kupigania haki hadi katika usimamizi (Qawamah) na uchungaji kutoka katika mtizamo wa kisheria

4. Usaidizi na kusahilisha kazi ya mashirika ya kieneo na ya kimataifa ya haki za kibinadamu na wanawake yanayotafuta kuifisidi familia za Waislamu, yanayotekeleza shughuli zao chini ya guo la haki za wanawake na watoto kwa hivyo yanapenya katika mashule na vyuo vikuu, yakipenyeza fikra za sumu miongoni mwa wanafunzi wake, na kuandaa hafla angamivu na amali zenye madhara kwa familia na mujtamaa. Yanaingia majumbani na kupigia debe mipango ya uzazi ili kuiwekea mipaka familia chini ya mwito wa afya na usalama wa wanawake, kuipiga vita familia ya wake wengi na ndoa ya mapema, na kupambana na fahamu ya ulezi chini ya bendera ya haki za wanawake, kutambulika kibinafsi na uhuru wa maamuzi, kuzuia udhibiti na utawala wa wanaume juu yake.

5. Kuidhinisha na kukubali mikataba ya kimataifa inayolenga nidhamu ya kijamii katika Uislamu, ikiwemo kadhia ya ndoa na familia, kama mkataba wa CEDAW, ambao masharti yake yanalingani uhuru wa kuanzisha mahusiano haramu baina ya vijana wa kiume na wa kike chini ya kisingizio cha uhuru wa kibinafsi. Pia unalingania usawa kamili baina ya wanaume na wanawake, kuondolewa kwa ndoa kwa mujibu wa vipengee vya sheria ya Kiislamu na kutabanni ndoa za kiserikali, kuondolewa kwa usimamizi (Wilayah) wa baba juu ya watoto wake, hususan wa kike, na mambo mengine yanayo kiuka vipengee vya Uislamu.

Hizi ni baadhi ya njia na mbinu zinazotumiwa na serikali zinazo tawala katika nchi za Waislamu ili kuifisidi familia za Waislamu katika jaribio la kuzitia usekula; hivyo basi, kutia usekula katika biladi za Waislamu kwa jumla. Hili lahitaji msimamo makinifu kwa kila Muislamu mwenye ikhlasi na makini katika Dini yake na Ummah kutibua njama hizi na maovu haya. Na inawahitaji kufanya kazi kwa ikhlasi na kwa nguvu kuileta dola inayotutawala kwa kitabu cha Mola wetu, kusimamia mambo yetu, na kuhifadhi mujtamaa na familia zetu. Dola hii ni Dola ya Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume, ambayo ni ahadi ya Mola wetu Ta'ala, na bishara njema ya Mtume wetu (saw).

Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

Bara'ah Manasrah

Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake na Watoto Janga Lilioletwa Kutoka Magharibi ya Kisekula



Kuenea kwa ghasia ndani ya ndoa kumekuwa ndiyo ada kwa kuendelea kuongezeka kwa idadi ya wanawake na watoto katika biladi za Waislamu. Hususan, mbio za kuiga muondoko wa kimaisha na utawala wa Kimagharibi, ghasia za kinyumbani zimesababisha kiza kizito kinacho ongezeko juu ya mujtamaa za Waislamu.

Kuvunjika kwa kiini cha familia, na hivyo basi hadhi na utulivu wa maisha ya kijamii katika ardhi za Waislamu ni natija ya yakini inayotokana pakubwa na kupigia debe fahamu na maadili ya kisekula ya kibinadamu yaliyoundwa na mfumo wa Kimagharibi wa kirasilimali. Mfumo huu hudai kuwa viwango ambavyo havina budi kutafutwa na mwanadamu ni maadili ya hali ya juu ambayo mwanadamu anajiwekea nafsi yake. Kwa msingi huo, hususan maadili ya Kimagharibi ya usawa wa kijinsia ni mojawapo ya fahamu msingi yaliyo enea katika mujtamaa na familia zetu kwa fitna zile zile za Wamagharibi wasiokuwa Waislamu. Zilifisidi mahusiano katika ndoa na maisha ya kijamii kupitia uhuru usio na mipaka na utafutaji matakwa ya kibinafsi; zilihujumu nukta zote za heshima, hali nzuri, hadhi kwa wanawake, watoto, na wanaume katika jamii. Wakati huo huo shutma kali za kisekula kwa sheria za kijamii za Kiislamu huziacha familia nyingi za Waislamu chini ya kinyongo cha kutapata.

Na ile dhana – kama aghalabu inavyodaiwa na wasomi wa kileo – kuwa muozo uchungu unaoendelea katika mujtamaa zetu ni kutokana tu na natija ya sera dhaifu juu ya wasiokuwa na talanta; ni makosa mno! Bali ni natija isokuwa na budi ya mfumo wa kirasilimali, ambao hauwezi kutatua kadhia nyeti za watu wake wenyewe. Hivyo basi ili kuhakikisha kubakia kwake, hauna chaguo jengine isipokuwa kuziba muozo wake pamoja na kuchafua na kuharibu utamaduni na miondoko ya kimaisha ya itikadi ya nidhamu nyenginezo. Kwa hayo haswa tatizo la ghasia katika mujtamaa zetu, hususan ghasia za kijamii, ni natija ya mradi muovu uliopangwa

kabla kwa muda mrefu ili kuzikoloni ardhi zetu, uliomakinika kupitia utekelezaji nidhamu za kiutawala, serikali zao, taasisi rasmi, vyama na mashirika ya kutetea haki za wanawake, ambayo ni vifaa vya dola za kikoloni vinavyo tumiwa kuwatawala Waislamu. Makala haya yatatoa ushahidi wa ukubwa wa ghasia katika familia na dhidi ya wanawake na wasichana zinazoenea katika ardhi zetu za Kiislamu.

Tunisia ndio nchi ya kwanza katika ulimwengu wa Kiarabu iliyo anzisha Kanuni ya Kileo ya Hadhi (CPS) mnamo 1957 iliyo badilisha sheria nyingi za kijamii na familia kwa zile zilizo jengwa juu ya usekula. Dola hii tiifu ya kisekula daima iliwakilishwa na serikali za Kimagharibi, watetezi wa wanawake na taasisi kama muundo wa kutafuta haki za wanawake katika ulimwengu wa Waislamu. Lakini, upigiaji debe na utekelezaji wa maadili huru ya kisekula, sera na kanuni ndani ya mujtamaa wake yamepelekea tu ongezeko la ukandamizaji kwa watu wake na hususan ghasia dhidi ya wanawake. Leo, nchi hii iliyo Kaskazini mwa Afrika kwa sasa ina moja wapo ya viwango vikubwa mno vya ghasia za kifamilia ulimwenguni huku utafiti ukionyesha kuwa karibu nusu ya wanawake wote ni waathiriwa wa uhalifu huu katika kipindi fulani cha maisha yao. Utafiti uliofanywa na Chama cha Kidemokrasia cha Wanawake cha Tunisia (ATFD, ufupisho wake kwa Kifaransa) umefichua kuwa asilimia 84 ya wanawake ambao ni waathiriwa wa ghasia wameolewa, na asilimia 82 ya kesi hizi hutokea katika nyumba zao za ndoa.

Afisi ya Kitaifa ya Familia na Idadi ya Watu imefichua kuwa takriban asilimia 50 ya wanawake wa Tunisia wameteseka kupitia baadhi ya aina za ghasia, na kwamba asilimia 42 yao wamehitimu chuo kikuu. Uchaguzi wa kiwango cha wastani cha wanawake 3000, ulionyesha kuwa asilimia 31 yao wamewahi kuwa waathiriwa wa ghasia za kimwili, asilimia 28 wamepitia ghasia za kijinsia na asilimia 7.1 walikabiliwa

Endelea Uk..19

na ghasia za kiuchumi (13 Agosti 2014). Mwaka huu, utafiti mwingine, uliochapishwa na Kituo cha Utafiti, Uchunguzi, Unakili na Habari juu ya Wanawake (Kundi la Kitunisia kwa ushirikiano na UN), liligundua kuwa asilimia 70 – 90 ya wanawake wamekuwa ni waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia, wengi wao wakiwa katika usafiri wa umma, kuanzia 2011 hadi 2015.

Chimbuko jengine la wasiwasi kuhusiana na usalama wa wanawake nchini humo ni usafirishaji wa wanawake. Kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM), Tunisia ni chimbuko, sehemu na nchi ambayo ni njia ya usafirishaji wanawake ambao “wanafanyishwa kazi kwa lazima na kusafirishwa kwa ajili ya ngono”.

Yote haya yanaonyesha kuwa kutabani kanuni kwa aina yoyote hakujafeli tu kuwalinda wanawake nchini Tunisia, bali kikweli imepelekea ukandamizaji mbaya na ongezeko la ghasia. Na bado, nchi hiyo inahamu ya kutekeleza zaidi maadili na kanuni za kisekula za Kimagharibi, kama kuanzisha usawa kamilifu wa kijinsia katika katiba yake, na “Sheria ya Kuondoa Ghasia dhidi ya Wanawake” ambayo inatarajiwa kutekelezwa mwaka huu.

Uturuki ni biladi nyengine ya Kiislamu iliyopewa misheni ya kuwa kiigizo chema kwa haki za wanawake na kuwa mwanzilishi katika kupigia debe na kutabikisha maadili ya kirasilimali kama usekula, demokrasia na usawa wa kijinsia katika ulimwengu wa Kiislamu. Uturuki imeshiriki kichangamfu takriban katika kila makubaliano ya kimataifa kuhusiana na wanawake. Iliidhinisha mkataba wa kimataifa wa UN, Kongamano juu ya Kuondosha Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) mnamo 1986, na kuasisi Kitengo Jumla juu ya Hadhi ya Wanawake (GDSW) kama mbinu ya kitaifa mnamo 1990 ambayo ilichangia pakubwa kushiriki kichangamfu kwa Uturuki katika Tangazo la Beijing na Jukwaa la Utendakazi juu ya michakato ya haki za wanawake mnamo 1995. Ilikuwa nchi ya kwanza iliyotia sainsi Kongamano la Kukinga na Kupambana na Ghasia dhidi ya Wanawake na Ghasia za Kinyumbani mnamo Mei 11, 2011 na kuwa nchi ya kwanza kuliidhinisha mnamo Novemba 25, 2011. Kupambana na ghasia dhidi ya wanawake kulitambulika kama sera ya dola hiyo na kukumbatiwa na taasisi nyingi za dola yake tangu 1995.

Ilhali vitendo vyote na juhudi zote hizi na miradi ya kupigia debe na kutekeleza usawa wa kijinsia ndani ya nchi hiyo vilizalisha **ongezeko la kasi la viwango vya ghasia dhidi ya mwanamke ulimwenguni**. Kwa mujibu wa Wizara ya Haki ya Uturuki, kuanzia 2003 (pindi chama cha APK kilipoingia mamlakani) hadi 2014, kulikuwepo na ongezeko la asilimia 1,400 katika idadi ya mauwaji ya wanawake. Na ni muhimu kutaja kuwa mabadiliko makubwa katika kanuni na sheria kwa mujibu wa makubaliano ya kimataifa kama CEDAW na Tangazo la Beijing yalifanywa na serikali ya APK.

Kwa mujibu wa TUIK (Taasisi ya Takwimu ya Uturuki), wanne kati ya wanawake kumi hukumbwa na ghasia za kinyumbani, huku Wizara ya Familia na Sera za Kijamii ya Uturuki ikiripoti kuwa asilimia 86 ya wanawake nchini Uturuki walipitia ghasia za kimwili au kisaikolojia kutoka kwa wapenzi wao au mwanafamilia mwenza. Zaidi ya wanawake 300 walikufa kutokana na ghasia za kinyumbani mnamo 2015 pekee. Mnamo 2014, mamia ya wanawake waliuwawa na wanandoa wenzao katili hata baada ya kuomba hifadhi ya polisi. Kwa sasa Uturuki inasimamia nyumba rasmi takriban 100 zinazowapa makao wanawake chini ya 3,000, huku mashirika yasiyo ya kibiashara yakilemewa na kung’ang’ana kuwachunga wanawake wengine 20,000 zaidi wanao tafuta makao kila mwaka. Ripoti hiyo ya shirika la wanawake (Kadın Cinayetlerini Durduracağız Platformu) lilifichua mauwaji 409 ya wanawake, kesi 387 zilizo rekodiwa za dhulma za kimapenzi kwa watoto, na kesi 332 zilizo rekodiwa za ghasia za kijinsia kwa wanawake mnamo 2017. Idadi inaongezeka kwa kasi kila mwaka. Zaidi ya hayo, la kuogofya zaidi ni habari moja kuhusiana na ghasia dhidi ya watoto. Mtindo mpya unaibuka katika kesi za talaka, ambapo kina baba huwauwa watoto wao wenyewe kama kisasi cha talaka wanayoikataa. Hivyo basi, watoto 20 waliuwawa na baba zao wenyewe mnamo 2017 pekee.

Idadi na ripoti kutoka katika biladi za Kiislamu, zinazo tawaliwa na serikali na nidhamu za kisekula au serikali na nidhamu nyenginezo zisizo kuwa za Kiislamu, zinaashiria sura kama hii: Nchini **Afghanistan** asilimia 80 ya wanawake wa Afghan wanapitia au washapitia kwa uchache aina mojawapo ya ghasia katika maisha yao (UNFPA 2016). Wizara ya Afya ya Umma ilisajili kesi 8,188 za ghasia za kijinsia ambapo kesi 2,806 zilikuwa za ghasia za kimwili, 3,470 dhulma za kisaikolojia, 1,207 ukosefu wa njia ya kufikia rasilimali, 403 ndoa za lazima, 166 dhulma za kimapenzi na 136 unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya wanawake. Wizara ya Mambo ya Wanawake ya Afghanistan ilitangaza takribani kesi 4,000 zilizo rekodiwa za ghasia dhidi ya wanawake mnamo 2017.

Karibu wanawake milioni 1.5 nchini **Misri** wanapitia ghasia za kinyumbani kila mwaka kwa kiwango cha zaidi ya kesi 4,000 kila siku (Baraza la Kitaifa la Wanawake nchini Misri / 2016). Nchini **Palestina**, takriban asilimia 37 ya wanawake ambao wameolewa washawahi kupitia aina mojawapo ya ghasia kutoka kwa waume zao (Utafiti wa Kitaifa juu ya Ghasia katika Jumuiya ya Palestina, 2011). **Indonesia** takwimu zake ni kama hizi zinazo eleza kwa ufupi kuwa kesi 245,548 za ghasia dhidi ya wake zilitokea mnamo 2016 pekee (Komnas Perempuan, 2016). **Malaysia** inafuata kuripotiwa kesi 10,282 za ghasia za kinyumbani mnamo Januari 2016 pekee (WAO, 2016). Kwa mujibu wa shirika la habari la BBC huduma ya Kifursi, asilimia 66.3 ya wanawake nchini Iran wamepitia ghasia maishani mwao (RUDAW, 2014).

Janga hili kubwa la ghasia dhidi ya wanawake na

Endelea Uk..20

JARIDA LA
UQAB

ghasia za kinyumbani ukweli ni kadhia iliyo ingizwa ndani ya ardhi zetu kutoka Magharibi inayoteseka yenyewe kutokana na janga la uhalifu kama huu kutokana na nidhamu yake ya kirasilimali, kisekula na thamani huru. Kwa mfano, nchini **Uingereza**, wanawake milioni 1.2 waliripoti dhulma za kinyumbani nchini Uingereza na Wales katika mwaka wa 2016, na mwanamke 1 kati ya 4 hupitia ghasia za kinyumbani. (Afisi ya Kitaifa ya Takwimu). Mnamo 2014, utafiti uliofanywa na shirika la Haki Msingi la Muungano wa Ulaya (FRA), lilifichua kuwa **thuluthi moja ya wanawake katika Muungano wa Ulaya washapitia ghasia za kimwili au za kimapenzi tangu umri wa miaka 15**, sawia na watu milioni 62. Utafiti huo kutoka nchi 28 za Ulaya pia uligundua kuwa 1 kati ya wanawake 10 barani humo ashawahi kuteseka kupitia baadhi ya aina za ghasia za kimapenzi na 1 kati ya 20 amebakwa, asilimia 55 walipitia unyanyasaji wa kimapenzi, aghalabu makazini, huku asilimia 75 ya wanawake waliofuzu taaluma au walio katika vyeo vya juu makazini wamepitia aina hii ya ukiukaji dhidi ya heshima yao, ikivunjilia mbali madai ambayo aghalabu hurudiwa kuwa ajira ni njia ya kuinua hadhi ya wanawake. Cha kuchekesha ni, **nchi zilizo na idadi kubwa zaidi ya matukio ya ghasia** zilikuwa ni **Denmark** (asilimia 52), **Finland** (asilimia 47), na **Sweden** (asilimia 46) – dola zilizo sifiwa kwa kanuni zake za usawa wa kijinsia na kutajwa kama nchi zilizo na usawa zaidi wa kijinsia kwa mujibu wa jedwali la Usawa wa Kijinsia la UN, ripoti ya Jukwaa la Uchumi wa Dunia ya 2013 na Taasisi ya Ulaya ya Usawa wa Kijinsia.

Na hizi ni baadhi ya takwimu kuhusu ghasia nchini **Amerika**, zilizochapishwa katika gazeti la 'Huffington Post' mnamo Aprili 5, 2017: Kila siku zaidi ya watu 570 hupitia ghasia za kimapenzi katika nchi hii ambayo imejaa takribani visa vya kila siku vya dhuluma za kimapenzi katika vitivo vya chuo, na kwamba hata inatawaliwa na Raisi ambaye ametuhumiwa hadharani akiwadhulumu kimapenzi zaidi ya wanawake 15. Takribani wanawake milioni 18 wamekuwa waathiriwa wa ubakaji tangu 1998. 1 kati ya wanawake 6 wa Amerika aliokoka na jaribio au ubakaji wa kihakika katika maisha yao. Idadi ya wastani ya waathiriwa wa ubakaji kwa mwaka inafikia hadi 321,500. Zaidi ya hayo, ghasia za kinyumbani ni za kawaida mno nchini **Amerika**, ambapo karibu wanawake milioni 5 hupitia ghasia za kimwili kutoka kwa mpenzi wake ... na kadhalika ... Kila aina ya dhuluma ya kimapenzi, ubakaji na aina nyengine za ghasia zaweza kupatikana viwango vya kutisha mno katika nchi hii, huku ikidai kuwa msimamizi wa haki za wanawake na binadamu.

Kiulimwengu wanawake na wasichana ni asilimia 80 ya makadirio ya watu 800,000 wanaosafirishwa kuvuka mipaka ya nchi kila mwaka, huku asilimia 70 yao wakisafirishwa kwa ajili ya kudhulimiwa kimapenzi. Hadi wanawake 7 kati ya 10 kwa mujibu wa ripoti ya dunia wamepitia ghasia za kimwili au za kimapenzi katika kipindi fulani cha maisha yao. Kote duniani

hadi asilimia 50 ya dhuluma za kimapenzi hufanywa dhidi ya wasichana chini ya umri wa miaka 16. Zaidi ya wasichana milioni 100 hupotezwa kutokana na kuchaguliwa kwa ngono. Na yote haya yamejitokeza huku mfumo huru wa kisekula wa kirasilimali unaotawala siasa za kimataifa na kitaifa leo na kujionyesha kutokuwa na fununu na kutokuwa na uwezo wa kusitisha wimbi hili la ghasia dhidi ya wanawake na wasichana. Zaidi ya hayo, mjumuiiko wa kanuni za usawa wa kijinsia, vifungu na miradi yake pamoja na mipango yake na sheria yake inayopigiwa debe kimataifa na kutekelezwa ndani ya dola za kimagharibi na za Waislamu ili kukabiliana na ghasia dhidi ya wanawake na wasichana imefeli waziwazi hata kupunguza mizani ya tatizo hili.

Mifano hii ya Waislamu na wasiokuwa Waislamu yaonyesha kuwa maadili huru ya kisekula ya urasilimali, yanayo shajiisha watu binafsi kutekeleza matamano na matakwa yao na ambayo sekta za burudani, zimeidunisha hadhi ya wanawake na kupigia debe uhuru wa ngono ambao unaufisidi na kuudhuru uhusiano baina ya jinsia ndani ya mujtamaa na imechochea moja kwa moja kudunishwa, kudhalilishwa na tabia ya ghasia dhidi ya wanawake kote ulimwenguni. Zaidi ya hayo, ukosefu wa hukmu na sheria za kukinaisha na kuridhisha ili kupangilia mambo na maingiliano baina ya wanaume na wanawake pamoja na ukosefu wa adhabu stahiki kwa wakiukaji wowote dhidi ya heshima na hadhi ya wanawake ilipelekea kukolea kusikodhibitika kwa ghasia dhidi ya wanawake. Maadamu maadili haya na mitazamo hii fisidifu itabakia ni yenye kutawala katika jamii zetu, kuunda sera chache au kanuni au kuunda miradi na mashirika ya wanawake daima zitafeli kuzungumzia tatizo hili. Badala yake zitaendeleza tu hali halisi, kuhifadhi utawala na uwepo wa nidhamu ya kiitikadi yenye kudhuru itokayo kwa mkoloni na miundo katika ardhi za Waislamu, ikiongeza zaidi uhalifu unaokiuka heshima na hali nzuri ya wanawake, na kuharakisha uharibifu wa muundo wa kijamii wa jamii za Waislamu.

Suluhisho pekee la janga hili ni kupinga kwa ujumla nidhamu mbovu za uhuru za kisekula zilizo lazimishwa juu yetu na wakoloni wa Kimagharibi wa kirasilimali na kuunda mustakbali wa ardhi za Waislamu juu ya mfumo wa Kiislamu pekee.

فَلْأَتَعْلَمُونَ اللَّهَ بِدِينِكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“Sema (ewe Muhammad): ‘Je, munamfundisha Allah kuhusu Dini yenu (mfumo kamili wa maisha) na ilhali Allah anajua vilivyomo ndani ya mbingu na vilivyomo ndani ya ardhi; Na hakika Allah ni mjuzi wa kila kitu.’ [Al-Hujraat: 16]

Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

Zehra Malik

Email: info@uqab.or.ke

Michezo ya Runinga: Kiwanda Kinacho Sambaza Uovu wake Juu ya Familia na Jamii!

TV Series

Michezo ya runinga imekuwa maarufu miongoni mwa watu wa umri wote walio na tofauti katika kupenda kwao. Idhaa za michezo ziko makini kupeperusha michezo tofauti tofauti mfano filamu za kawaida, filamu za kisasa, filamu za utafiti pamoja na michezo ya kuendelea katika runinga kuanzia ya kijamii hadi ya vichekesho, mapenzi na ngono, michezo ya kitoto na vipindi vya mfululizo kiasi kwamba kila vioo vya runinga vilivyo na vipindi hivyo vimekuwa marafiki wa kila mwanachama wa familia kwa kutegemea anachopenda na kutamani. Hasa nyakati hizi za maendeleo ya kiteknolojia, runinga za mfululizo na vipindi haviko tu katika runinga bali pia vinapatikana katika angavu.

Hii michezo na vipindi vya mfululizo-hususan vilivyo tafsiriwa-havikosi fikra ngeni na maadili juu ya thaqafa ya Kiislamu ambayo yanagonga na maadili ya Kiislamu na mizizi ya misingi yake na inalenga kujenga fikra jumla ndani ya ardhi za Waislamu ili ziwiane na fikra na fahamu za Kimagharibi na kuchukua zile zilizo oza ili ziweze kupigiwa debe ndani ya jamii zetu kama za kimaumbile na kawaida na kwamba inafuatiwa na Sera ya vyombo vya Habari ndani ya ardhi za Waislamu, ikilenga familia na jamii ndani ya ardhi za Waislamu.

Twaona kwamba katika hizi filamu za mfululizo kwa mfano zinashajiisha mchanganyiko kati ya wanaume na wanawake, na kuufanya kuwa ndiyo maisha na hitajio

la zama hizi, na tunapata kuwa inashajiisha tamaduni ya kuwa uchi na uzinifu ndani ya wanawake Waislamu, wakilifanya hilo kama kuenda sawa na mtindo na kuwa wazi kwa ulimwengu. Pia tunapata kuwa wanapigia debe mahusiano ya Haramu kati ya wanaume na wanawake wadogo, wakiwafanya wakubali na kuvutiwa na "mapenzi". Fauka ya hayo, tunapata ishara ya kuanikwa kwa Munkar na vitendo vilivyo katazwa mfano kuoneshwa kunywa pombe kama kitu cha kawaida, pamoja na miito ya uhuru kamili na uhuru uso vikwazo na vidhibiti vya hukmu (Shari'ah), ikijumuisha sherehe na mila za kishirikina na kuabudu masanamu ambazo zinapenyeza hizi filamu na vipindi vya mfululizo hususan vya Kihindi.

Athari ya hizi filamu na vipindi vya mfululizo haikufungika tu katika fikra na fahamu zake lakini zimejitokeza katika tabia za kula na mavazi pamoja na mahusiano kati ya wanachama wa jamii na familia, lakusikitisha ni kuwa mashujaa wa sinema hizi wamekuwa ndiyo wakuigwa na baadhi ya watoto Waislamu, kujifananisha nao katika mavazi, kunyoa, matembezi na tabia, na hata majina yao wakiwataja watoto wao!!

Tukiangalia hali za wanawake ndani ya michezo hii, tunawaona wakiwasilishwa kwetu katika sura zifuatazo: ima akiwa hana uwezo na ni mwenye kukandamizwa na hana udhibiti juu ya chochote na hana thamani katika

Endelea Uk..22

JARIDA LA
UQAB

jamii, katika muktadha huu jukumu kuu la wanawake kuwa mama na mke nyumbani linapigwa vita na kuoneshwa sababu za kupata shida kwake. Mwanamke anaoneshwa kama aliye kandamizwa na kutaabika kwa sababu ni mwanamke aliye kifungoni ndani ya nyumba yake. Hana kazi isipokuwa kuangalia nyumba yake na kulea watoto wake, na hivyo basi, imepandikizwa katika akili za wanawake kuwa suluhisho la matatizo yao lipo katika kuleta uasi dhidi ya jukumu hilo na kazi zilizomo ndani yake. Katika picha ya pili, amewasilishwa kama mwenye uwezo wa kushindana na wanaume na kusimamia mambo yake na kujitosheleza mahitaji yake na kufanya maamuzi yake kibinafsi, kwa kuwa yuko huru katika vitendo vyake, na anafanya anavyotaka bila mipaka. Hakuna vidhibiti juu ya mzunguko wake na kila kinachoweka kikwazo kwa uhuru wake anakiweka nyuma yake.

Yeyote anayefuatilia michezo ya runinga ataona kwamba wanatengeneza hadithi za mapenzi na ngono kama muongozo jumla, wakizipeana katika njia ambayo ni kinyume na uhalisia na kuwasilisha picha za uongo ambazo hupelekea katika kuunda ruwaza ya makosa kwa wale wanaotaka kuoana kwa maisha ya ndoa, ambapo mtizamo wa maisha ya ndoa ni wa kukamilika na uliojaa mapenzi bila kujali majukumu ya ndoa, na kwamba maisha yana uzito na mashaka. Mume katika filamu na vipindi hivi ni mtanashati, mtu wa kisasa, kijana na tajiri anayemletea zawadi mkewe ima ni au si siku adhwimu, na mke naye anaoneshwa kama mrembo, mwenye mvuto, asiye kuwa na shughuli bali kuhudhuria sherehe, vilabu na kusafiri na mumewe kama ambaye mwanamke huyu hana majukumu au kazi za kifamilia, na kama ambaye mume huyu hajui gharama yoyote, jukumu lolote na hana usimamizi wa watoto. Natija yake ni kuwa vijana hawa muda si mrefu wanakuja kugongana na uhalisia, majukumu na kazi zilizowekwa juu yao na kufungua mlango wa matatizo na mizozo ya ndoa ambayo hatima yake ni kuelekea katika talaka. Huu ni kwa mtizamo huu.

Kwa upande mwingine, wanaume na wanawake wadogo wanatafuta vigezo maalumu katika wale wanaotaka kuoana kwa mtizamo wa uwezo wa kimuonekano na kimada unaowasilishwa na sinema hizi. Huu ndio utangulizi wa kufeli kwa maisha ya ndoa kwa sababu kila mmoja anatafuta muonekano bila kujali msingi, na kila mmoja anatafuta yule atakayeishi naye “hadithi ya mapenzi” kama alivyoona katika sinema, na sio kutafuta mtu kwa mujibu wa Dini na akhlaq, mtu ambaye utaishi naye kwa mapenzi, kuhurumiana na utulivu, kama alivyosimulia Allah (swt) ndani ya kitabu Chake katika Surat Ar-Rum, aya 21:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً
وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

“Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye

amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya zipo Ishara kwa watu wanao fikiri”

Njia hii ya kufikiria haikufungwa tu kwa wale wanaotaka kufunga ndoa, bali hata kwa wale wanandoa. Wafuatiliaji wa michezo hii hususan wanawake huyapata maisha yao ni ya upweke na kushughulishwa na maisha yaliyowasilishwa katika michezo hiyo ambayo inapelekea katika mizozo na matatizo ya ndoa ndani ya majumba.

Hii ni sehemu tu ya fikra za sumu na chuki zinazopeperushwa na michezo ya runinga miongoni mwa watoto Waislamu, ambayo inalenga kufisidi Ummah kwa kupeana fahamu za Kimagharibi na kuzibadilisha fahamu za Kiislamu kuhusiana na mahusiano tofauti tofauti, mfano kati ya mahusiano ya wanaume na wanawake kwa kuzizungumzia mada ambazo zimetokana na Wamagharibi na watawala wao mfano mada kuhusu “ugaidi,” na kuwasilisha maisha ya Kimagharibi kama maisha ya kivyake ya kufuatwa. Wanaounda, kuziongoza na kuzipiga picha hizi sinema katika maeneo mazuri na yenye kuvutia mno na majengo yenye kuvutia na yaliyo ghali, mitindo na miziki yenye mvuto, pamoja na kuchezea hisia zote za uzuri wa mwanadamu ili kuweza kuathiri watazamaji, hususan watu wachanga.

Hivyo basi, lazima tuwe makini na vyombo vya habari na vinavyopeperusha, ima ni michezo au mengineyo, kwa makini na uangalifu ni lazima tusiwawache watoto wetu wakiume na wakike Waislamu watumike kama chombo katika mikono yao au chambo rahisi katika midomo yao. Hivyo basi, tunatoa mwito kwa wazazi kushirikiana katika kuzisimamia familia zao na kuwalinda kutokana na vyote vinavyo fisidi na kuwapa sumu, Allah (swt) asema ndani ya Surat At-Tahreem, aya 6:


يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قُوا أَنْفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ عَلَيْهَا
مَلَائِكَةٌ غِلَظٌ شِدَادٌ لَا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ

“Enyi mlioamini! Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrisha.”

Imeandikwa Kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

Bara'a Manasra

Mawasiliano ya Kieletroniki Yalivyo Vunja Majumba Yaliyokuwa Makini na Kuwatenganisha Watu!



Japokuwa mawasiliano ya kieletroniki ya habari yamefupisha masafa, yamekuwa njia fupi ya kupelekea talaka na mizozo ya ndoa. Na japo ilitumika kuwaunganisha wapendanao na wasiokuwepo baada ya kusubiri kwa muda mrefu, inawatenganisha wanachama wa familia na kuwasaidia kuwavunja kabisa, hakika ni jambo la utata mno!

Namna mitandao ya kieletroniki ya mawasiliano ilivyogeuka na kuwa laana baada ya kuwa baraka?!

Vyombo vya Habari vimebadilisha tabia na muundo wa matangamano baina ya watu, na chini ya mapinduzi ya kiteknolojia, watu wengi walianza kuugua upweke, kutengwa na jamii na msongo wa mawazo. Majumba zamani yaliyokuwa hai kwa gumzo la familia sasa yako kimya kama ambaye ni matupu hawamo, na ziara kwa ndugu na majirani siku adhwimu na likizo zimebadilishwa na jumbe na picha. Na kelele zilikuwa zikijaa ndani ya majumba ya mababu/nyanya kutokana na kujumuika kwa watoto na wajukuu, ile nishati, mizunguko na urafiki haupo tena. Kila mmoja anakuja akiwa amebeba kifaa chake na baada ya kujuliana hali, kila mmoja hujiweka kipembeni mwa nyumba, huku kiwiliwili chake chaishi na familia, lakini roho na akili yake haipo!

Kutokana na kusambaa kwa mitandao ya kijamii, majumba yamekuwa bila mipaka na stara imeondoshwa kutoka katika maisha ya watu na familia. Siri za majumba mengi zimekuwa wazi kwa kila mtu na kila hatua ya maisha yao ya siri yamepeperushwa, ikisababisha matatizo mengi ya kifamilia, mfano talaka na mizozo ya ndoa pamoja na wivu, kijicho na vita kati ya watu katika jamii.

Kwa mujibu wa utafiti na ripoti, mitandao ya kijamii hususani Facebook na WhatsApp ndiyo vyanzo msingi vya kuwepo kwa viwango vya juu vya talaka. Hatuwezi kuweka takwimu zote hapa lakini wacha tutaje tu baadhi ya ushahidi unaoonesha ukubwa wa tatizo hili ili kuzinduana. Ndani ya Palestina, mahakama za Sharia zimesema kuwa nusu ya kesi za talaka zinatokea kabla sherehe ya ndoa, na wajuzi wanatoa sababu kadhaa kwa hili; kwamba ya juu zaidi ni mawasiliano ya kimitandao. Kwa mujibu wa takwimu zilizopeperushwa mnamo 2016, miaka mitatu iliyopita imeshuhudia kuzidi kwa idadi ya talaka ndani ya Jordan, inayozidi kila mwaka kwa zaidi ya kesi 1000 kutoka zile za mwaka wa awali, tukizingatia kuwa njia za mawasiliano ya kisasa, Facebook, WhatsApp, ndiyo sababu kuu za kuzidi kwa kesi za talaka. Tafiti zaashiria kuwa mitandao ya mawasiliano ilisababisha asilimia 50 za kesi za talaka UAE. Kitengo

Endelea Uk..24

cha Muongozo wa Familia ndani ya UAE inakadiria kuwa mizozo ya ndoa ilizidi kwa zaidi ya kesi 5000 mnamo 2015 ambazo kuanzia asilimia 50 hadi 60 zinahusiana na mitandao ya kieletroniki na 1000 kati ya hizo ziliishia na talaka.

Takwimu na ushahidi huu wa kushtusha unaonesha namna hii mitandao na aplikesheni za simu za mkono zinavyosababisha mizozo ya ndoa kwa wale ambao wanairuhusu imiliki maisha yao; kwa upande mwingine kwa kumtenganisha mtu na familia yake na kumfanya asitekeleze majukumu yake juu yao hususani ikiwa mtu huyo ametekwa na matumizi yake na kuchukua muda mwingi nayo sawa na au kupitiliza muda mzazi anaotumia na watoto wake, au wanandoa wanaotumia ambayo ni ya kushtusha kwa hali nyanja zote mbili. Kutekwa huku kunawafanya wazazi kufeli katika utendaji wao wa kazi juu ya watoto wao katika elimu, kuwaongoza, kuwapa upendo na mapenzi yanayostahili na kuwasikiza wao na matatizo yao ambayo inapelekea kwa watoto kuchukua muelekeo hatari na kuwafanya waanze kuwa na tabia mbaya, kando na thaqafa iso madhubuti na fahamu za makosa ambazo watoto wanasoma kama natija ya kutumia muda wao mwingi katika mitandao hii na ilhali wazazi wao hawajui kuihusu.

Kwa wanandoa, kutekwa huku kunapelekea kutelekeza na mawasiliano mabaya kati ya wanandoa na kufeli kufanya kazi zao kuelekea upande mwingine, na wakati mwingine mmoja kati ya wanandoa hao hupata ndani ya vyombo hivyo vya habari kama sehemu ya kujificha ili asitumie wakati wake na mwenzie kwa sababu baadhi ya matatizo baina yao yanapanua pengo na kuzidisha mizani ya matatizo.

Kwa upande mwingine, mitandao hii na aplikesheni zake zimewezesha mawasiliano na kuzalisha mahusiano na kubadilishana kwa jumbe na picha kati ya wanaume na wanawake ambayo imepelekea –kukosekana kwa uchajiMungu na kumuogopa Allah (swt) –kumepelekea viwango vikubwa vya usaliti, ambayo ni moja ya sababu ya viwango vikubwa vya talaka kama ilivyodhibitishwa na rekodi za Mahakama ambazo ziko juu kutokana na kesi za talaka kwa sababu ya usaliti.

Urahisi huu wa mawasiliano umesababisha wanandoa wengi kupoteza uaminifu kati yao, ambacho ni moja kati ya misingi muhimu ya mahusiano mazuri ya ndoa, ikiwasababishia baadhi yao kuishi katika hali ya kushuku na kutoamini upande mwingine. Inaweza kumsukuma mmoja wa wanandoa kufuatilia na kuchunguza yote yanayomfikia mwenzake kupitia mitandao hii na aplikesheni zake na kufuatilia wanaotuma.

Mazungumzo kuhusu suala hili ni marefu na yakusikitisha, lakini twamalizia kwa kusema kuwa mawasiliano ya kieletroniki yameunda urongo na kupanua pengo ndani ya mahusiano ya kifamilia kati ya dunia mbili: moja ambayo ni ya kweli, na nyingine

ambayo si kweli, inayoathiri vibaya mahusiano ya kifamilia na kuzidisha pengo kati ya wanachama wa familia. Hivyo basi, jotojoto na ukaribu wa wanachama wa familia umekosekana licha ya kuwepo kiwiliwili, ambapo wanashikilia simu zao bila kujali wamekaa na nani; hivyo basi watu walisambaza misemo mfano: “Njia za mawasiliano zilisitisha mawasiliano.” Natija ni kuwa na sura mbili ambapo mahusiano ya kweli yamepungua na mahusiano ya tarakilishi yamezidi kwa hiyo urafiki na mahusiano yamepanuka kieletroniki lakini yamepungua mashinani na hisia za kinafiki na za uongo zimeibuka miongoni mwa wanachama wa familia moja, na hata miongoni mwa wanachama wa jamii jumla

Miongoni mwa natija zake ni kukosekana kwa utulivu katika majumba na kusitisha kwa mkataba ambao Allah (swt) ameelezea ndani ya Kitabu Chake wazi, Alisema:

وَكَيْفَ تَأْخُذُونَهُ وَقَدْ أَفْضَى بَعْضُكُمْ إِلَى بَعْضٍ وَأَخَذْنَ مِنْكُمْ مِيثَاقًا غَلِيظًا
“Na mtachukua je na ilhali mmekwisha ingiliana nyinyi kwa nyinyi, na wao wanawake wamechukua kwenu ahadi iliyo madhubuti?” [An-Nisa: 21]

Ndugu na dada ni muhimu kuyafanya mawasiliano ya kieletroniki kama Baraka inayotuunganisha na kutuleta karibu, na sio laana inayo vunjia majumba yaliyokuwa makini na kuwatenganisha watu wake.

Imeandikwa Kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

Bara’ah Manasrah